

NYAKATI SABA ZA KANISA

 ...Bwana Yesu Mbarikiwa. Nami ninazitazamia ibada hizi za usiku kwa hamu kubwa, nikitumainia ya kwamba kwa namna fulani, kwa njia fulani, ya kwamba Baba yetu wa Mbinguni atatutunukia baraka Zake. Na mara kwa mara ninapata nafasi ya kuingia kufanya ibada hizi hapa ka—kanisani, pamoja na kundi hili, enyi kundi dogo ambao ni washiriki wa hapa kanisani, na wageni, bila shaka.

² Na huu haukutangazwa. Ulikuwa tu ni mkutano wa kawaida wa maombi ya Jumatano usiku. Nami nilisema, “Labda usiku huu tuone kama tutarudi.” Nami nilifikiri tulikuwa tumeuchukua, labda, na kuutangaza kwa ajili ya juma lijalo, mbona, ingekuwa... Hatuwezi kuketi watu wengi sana hapa.

³ Na ibada za namna hii, Mungu akipenda, hazielekezwi kwenye... Zinaelekezwa kwenye Kanisa, kwa manufaa ya Kanisa, mahali ambapo tunaona kwamba zinahitajika sana kwa wakati huu, kila mahali, ni, pia, kwa ajili ya kuujenga kiroho Mwili wa Kristo. Na, sasa hili, katika kufundisha. Nimekuwa na ibada za kuponya kwa miaka minane, moja kwa moja; na basi, mafundisho, yatakuwa kwa namna fulani ni jambo jipya.

⁴ Basi nilikuwa ninawazia, alasiri ya leo, nilipoifungua Biblia, baada ya kuwa na shughuli nyingi sana siku nzima. Niliwaza, “Vema, niliwaambia watu ningefundisha juu ya *Nyakati Saba Za Kanisa*, labda, Bwana akipenda.” Nikaanza kusoma, na, nikalipata hilo tu, nikafurahi sana, wakati nilipoanza kulisoma. Ndipo nikawaza, “Vema, ninaweza kuchukua yote hayo katika usiku mmoja, katika saa moja.”

⁵ Kwa hiyo, sikujua jambo ambalo Roho Mtakatifu angetutaka tufanye. Sisi, sisi hatujaribu kupanga cho chote. Ni tu, “Kama ni mapenzi Yako, Bwana,” mnaona. Hilo ndilo jema zaidi ya yote. Na basi, kama ni mapenzi ya Bwana, ningetaka kufundisha usiku huu juu ya nyakati za kanisa, na kesho usiku juu ya *Alama Ya Mnyama*, na usiku ufuatao juu ya *Muhuri Ya Mungu*, na jambo hilo.

⁶ Na, halafu, Jumamosi. Ndugu yangu, bawabu, alikuwa hivi sasa akiniambia, leo; alisema, “Kama wangelikuwa nayo Jumamosi usiku na Jumapili asubuhi, kwa kawaida, wakati wageni wanapokuja miongoni mwetu, mbona, kanisa lingekuwa chafu sana, na kadhalika.”

⁷ Kwa hiyo wao wakashauri tu kuwa na Jumatano, Alhamisi, na Ijumaa, na Jumapili asubuhi, Jumapili usiku. Ndipo nikasema, “Vema, hilo lingekuwa sawa kabisa, nionavyo mimi.”

⁸ Kwa hiyo basi tutajaribu, Bwana akipenda, kuufanya Jumatano, Alhamisi, na Ijumaa, na Jumapili asubuhi, na

Jumapili usiku. Na, labda, Jumapili usiku tunaweza tukawa na ibada ya ubatizo, kwa kuwa watu tayari wamekuwa wataka kubatizwa. Na kwa hiyo sasa . . .

⁹ Nasi tutajaribu, kila usiku, na tuanze kwa wakati mzuri, kwenye saa moja na nusu. Nami nitakuwa jukwaani kwenye saa mbili, tunapaswa kuwa tumetoka kwenye maskani kwenye saa tatu na nusu, Bwana akipenda. Ili kwamba ninyi . . . Najua mnafanya kazi, nasi tunaliheshimu jambo hilo.

¹⁰ Na sasa Jumbe hizi ndogo kutoka kwenye Kitabu cha Ufunuo zinaelekezwa kwenye Kanisa. Nami ningependa kwamba kila mtu akumbuke jambo hili, ya kwamba hazielekezwi kwenye dini ya mtu, wala kwenye kusudi lingine lo lote; ni tu, ni juavyo mimi, kwenye kusoma na kueleza Neno la Mungu. Mnaona? Si kwa kusudi lo lote la kichoyo, wala haelekezwi kwa mtu ye yote, mtu ye yote binafsi, au kanisa la mtu ye yote, dini ya mtu ye yote.

¹¹ Na sababu ya mimi kupenda kufundisha juu ya ufunuo huu hapa maskanini, kwa kuwa ni kanisa langu mwenyewe, mbona, ninajisikia tu kana kwamba niko nyumbani. Na—nami tu, mwajua, kwa namna fulani nawapa kondoo wangu namna ya chakula nilichofikiria walikihitaji, mwajua. Baadhi ya . . .

¹² Watu mara nyingi inawabidi kutia chumvi kidogo wakati a—a—alfalfa kidogo imeshikwa na kuvu, mwajua. Huenda ikawadhuru kondoo usipofanya jambo hilo. Kwa hiyo, mara kwa mara, wakati labda alfalfa kidogo imeshikwa na kuvu kanisani, na—na tofauti ndogo ndogo zinazuka, basi nafikiri chumvi kidogo, kwa namna fulani, inatia ladha. Sivyoo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Kwa namna fulani inawakinga na maradhi.

¹³ Kwa hiyo sasa tunaomba ya kwamba—ya kwamba Mungu atatubariki katika jitihada hizi. Basi ni wangapi wanajisikia tu, kama tu wanaume na wanawake, kama tulivyo sisi, ningetaka kuliangalia jambo hilo, kesho usiku, juu ya, “Alama ya mnyama ni nini?” Kuna mengi sana juu yake katika Biblia. “Ni nani aliye nayo? Na ni nani atakayekuwa nayo?”

¹⁴ Na halafu, jambo lingine, unakuja wakati ambapo kitu hicho kitakuweko. Nami sijui, huenda ikawa ni wakati huu. Tutaangalia tuone. Ya kwamba, kutakuwa na tabaka mbili tu za watu duniani, na moja itatiwa alama ya Ibilisi, na hiyo nyingine alama ya Mungu. Nami nafikiri, ya kwamba kama tunaukaribia wakati huo, afadhali kwa namna fulani tuanze kuangalia kila mahali, tupate kujua kitu hicho ni nini, kwa maana bila shaka hakitaingia tu kama kitu fulani kikubwa mno. Biblia ilisema kingeingia kisiri kwa urahisi sana, hata, “Ingewapoteza walio wateule kama yamkini.” Kwa hiyo tutajaribu, kama Mungu akipenda, kuliangalia jambo hilo, kesho usiku. Sasa hiyo ndiyo njia bora sana ya ninii yangu . . .

15 Sasa, njoni na Biblia zenu, na penseli zenu na karatasi, nanyi mnataka kuandika Maandiko. Na, iwapo hudhani jambo hilo ni kweli kabisa, niandikie kijikaratasi kidogo ukiweke hapa kwa ajili ya usiku ujao.

16 Ninakumbuka nikikaa mwaka na miezi sita katika Kitabu hiki cha Ufunuo, ma—maskanini hapa. Hilo ndilo ninalopenda, katika—katika kufundisha. Ninapenda sana kufundisha. Loo, jamani! Na—na—nafikiri ni jambo zuri sana. Kuweka msingi, na kunaimarisha kanisa.

17 Na—na, kuhubiri, sasa, kuna watu ambao ni wahubiri. Wao wanaweza kuchukua Neno, kwa uvuvio, na kulitikisa huko nje mahali fulani. Huko ni kutia maji Mbegu ambazo mwalimu amefundisha. Mnaona? Sasa, huna budi kupanda baadhi ya Mbegu, kwanza, kisha uzitie maji. Nako kutia maji kunatokana na kuhubiri Neno.

18 Kuna tofauti kubwa, kubwa mno kati ya mwalimu na mhubiri. Mnaona? Ni karama mbili mbalimbali za Roho, kwa jumla, karama mbili mbalimbali. Nami nasema jambo hili kwa unyenyekevu, lakini, mimi sina karama mojawapo ya hizo mbili.

19 Lakini yangu, kama kawaida, ni kuwaombea wagonjwa. Hilo ndilo Mungu aliloniitia nifanye. Halafu basi, katika wakati huu, linanipa kupumzika akili zangu, kujifunza kitu fulani tofauti, si kuwa na ibada za kuponya Kiungu; ku— kufundisha tu Neno. Na, loo, tunaendelea vizuri sana hapa. Sisi. . .Ninakumbuka, mmenivumilia kwa muda mrefu, yapata miaka kumi na miwili hapa, juu ya jambo hilo.

20 Nami nilizoea kusema, bali sikulikusudia kama utani, lakini, kufundisha kunaparuzi sana, nikasema, “Ni kama tu jamaa fulani aendae mezani na kula ugali wa mahindi na maharagwe.” Naam, ni jambo zuri kwako, bali linakuchosha kidogo, mara kwa mara. Bali unaweza kuwa na kitu fulani pembeni, aisikrimu kidogo na keki, mara kwa mara, lakini kwa namna fulani hilo linasawazisha chakula. Bali kile kitu cha mtindo wa kale kitakaa nawe vizuri sana, na, hata hivyo, kinakupa mwamsho fulani.

21 Sasa, katika jambo hili, ninaamini kwa unyenyekevu wa imani yangu ya kwamba tunaishi katika siku za kumalizia historia ya ulimwengu. Ninataka kufanya jambo hilo dhahiri sana. Sasa ningeweza kukosea. Sijui. Hakuna mwingine ajua. Yesu alisema, “Hata Malaika wa Mbinguni wasingejua.” Yeye hakujua, Yeye Mwenyewe. Alisema, “Hilo ni kwa njia ya Baba tu, Yeye Ndiye tu anayejua.” Bali ni hakika na ni jambo la kweli kwamba Yeye anarudi. Nami siwezi kuona kitu kingine kilichosalia ila kule Kuja kwa Bwana.

22 Wakati, ninapotazama na kuona, taifa limevunjika. Ninaona siasa zimevunjika. Ninaona nyumba zimevunjika. Ninaona kanisa limevunjika. Sasa, hakuna kitu kingine kingeliweza kulitengeneza, ila Mungu, basi, maana wao hawana kitu kingine.

Uadilifu wa taifa umevunjika. Pia vyama vya siasa vimevunjika. Vema, tulitumainia sana siasa zetu; zimevunjika.

²³ Basi mtu fulani mashuhuri huko Uingereza, si muda mrefu uliopita, alisema, “Vema, demokrasia ilikuwa—ilikuwa matanga matupu bila nanga.” Hilo lilimaanisha, “Utakuja wakati watakaposimama juu ya masanduku ya sabuni, wakitafuta kura.” Vema, hiyo ni kweli. Bali yeye hakufikiria juu ya Baraza lake la Wabunge analolipenda, jinsi lilivyokuwa matanga matupu bila nanga, pia. Nalo liliruka, pia.

²⁴ Na kila ufalme wa dunia hii utavunjwa vipande-vipande. Yesu Kristo atatawala na kumiliki. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kuna . . .

Tumaini langu halijajengwa juu ya kitu ila

Damu ya Yesu na haki;

Kila kitu karibu na nafsi yangu kikivunjika,

Yeye ndiye tumaini na tegemeo langu.

Kwake Yesu, Mwamba wenye imara,
nasimama,

Mahali pengine pote ni mchanga udidimiao.

²⁵ Na, loo, jinsi ninavyotamani kama tungalikuwa tunaanza ibada ya kama miezi mitatu ya mafundisho, ili kwamba mweze kuingia katika Kitabu cha Ufunuo na kukiunganisha na cha Danieli, lile ono kuu.

²⁶ Ni wangapi waliosalia, katika hili kundi dogo hapa, ambao walikuwa wanakumbuka wakati nilipokuwa na ile ramani ya zamani hapa? Ninajua Ndugu Head alikuweko, nasi tulikuwa na wengi wenu hapa wakati walipokuwa na ile ramani ya kale.

²⁷ Sasa, Kitabu cha Ufunuo, jinsi kilivyoandikwa. Na cha Danieli kinashikamana Nacho. Isaya kinashikamana Nacho. Agano la Kale lote linashikamana Nacho. Nacho ni Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo. Mnaona? Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo.

²⁸ Na halafu, ndani humo, kuna Makanisa Saba, Mapigo Saba, Muhuri Saba, Baragumu Saba. Naam, baragumu huwakilisha vita; muhuri, siri inayofunuka; na pigo ndilo jambo linalofuata kila vita.

²⁹ Na kwa msaada wa Mungu, pamoja na kitabu cha historia, ninaweza kuwathibitishia ya kwamba tunaishi kwenye ile Baragumu ya Saba, kwa ajili ya lile Pigo la Saba, na ile Muhuri ya Saba kufunguliwa, na kile Kitasa cha Saba kumwagwa.

³⁰ Wakati ile ya sita ilipotoa sauti yake; tutafikia jambo hilo labda jioni ya leo, njia fulani, Ijumaa usiku. Wakati Vita vya Kwanza vya Dunia, mbona, ile . . . Baragumu ile ya Sita ilipigwa kulingana, kulingana hasa, na wakati Mungu aliponena habari zake. Hasa, kijiografia, kufuatia ile muhuri iliyoitangulia. Na wakati ile siri ilipofunuliwa mle ndani, kwa ajili ya ubatizo

wa Roho Mtakatifu; nao wale—na wale watu wakati huo, jinsi kanisa halikusonga mbele; na hao waliokuwa wanasonga mbele wakakataa kutembea katika Nuru, wakarudi nyuma. Ndipo pigo likafunguliwa wakati huo, na kumwagwa juu ya nchi, ambalo lilikuwa ni mafua, ambayo yaliwauwa watu kama yalivyofanya, wale maelfu mara elfu.

³¹ Halafu kushuka kuja katika wakati huu wa mwisho, mahali tulipo hapa. Ndipo tunakuja tu na kulisikiza yale Bwana anayotaka kusema juu ya jambo hilo, katika Neno Lake. Sasa, hilo si langu la kujibunia. Nitakuwa nikilisoma tu kama gazeti, moja kwa moja kutoka kwenye Neno la Mungu. Kwa hiyo, huu ni ufunuo Wake wa moja kwa moja kwa Kanisa, kwa Kanisa; Ufunuo wa Yesu Kristo, kwa Kanisa.

³² Basi kabla hatujazungumza Naye, ama kuzungumza juu ya maandiko Yake, hebu tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza Naye kwa muda kidogo tu katika maneno machache ya maombi.

³³ Baba yetu mwema wa Mbinguni, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa uchaji mavumbini, tulikotolewa na tutakakorudi siku moja, endapo utakawia. Tunaviinamisha kwa unyenyekevu, kukuomba ya kwamba utakuwa karibu nasi, usiku huu, kutubariki. Ninaweza kugeuza kurasa za Biblia hii, bali hakuna mtu anayeweza kukifungua hiki Kitabu wala kuifungua mihuri yake. Pia imeandikwa Humu ndani, “Yeye atakayeondoa kutoka kwenye Hiki, ataondolewa, sehemu yake, katika Kitabu cha Uzima; naye anayeongeza Kwake, mapigo ya Mungu yatamwagwa juu yake.”

³⁴ Baba, tukitambua, kama wanaume na wanawake wapatikanao na mauti waketio hapa usiku wa leo, tukijua ya kwamba sisi ni watu wanaoelekea Umilele. Mungu, Roho Mtakatifu na aje, mwandishi wa Biblia hii, na kutufungulia kurasa hizi. Pia mjalie mtumishi Wako mnyenyekevu na asiyefaa kuhubiri kama mtu anayekufa kwa watu wanaokufa, kana kwamba hii itakuwa ndiyo ibada ya mwisho nitakayopata kuwa nayo upande huu wa Umilele, usiku wa mwisho ambao tutawahi kukusanyika pamoja. Basi na kila mmoja wa wafuasi atende usiku wa leo kana kwamba haya yalikuwa ndiyo mahubiri yao ya mwisho watakayopata kusikia. Mungu, ondoa ujinga wote. Na utufanye waaminifu, tukijua ya kwamba hatuna budi kuwajibika kwenye Hukumu ya Mungu, siku moja. Na msimamo wetu Kwake na kwa Neno Lake, sasa, -taamua kikomo chetu cha Milele.

³⁵ Kwa hiyo, Baba, kwa mioyo inayotetemeka, tunakuja Kwako, na kuomba. Mjalie Bwana Yesu, katika namna ya Roho Mtakatifu, alichukue Neno la Mungu, usiku wa leo, na kulitoa kwa kila moyo, kulingana na mahitaji yetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

³⁶ Inaweza tu kuonekana kidogo ni jambo la kigeni kwangu, kwa dakika chache sasa, katika kujaribu kuanza kufungua somo la kufundisha. Kwa maana, imekuwa daima kwenye kuponya Kiungu kwa miaka michache iliyopita, halafu basi— halafu si katika unabii, la hashu, halafu—halafu kwenda moja kwa moja kwenye mstari wa maombi.

³⁷ Lakini sasa, usiku wa leo, tunataka kupata msingi wa kile Kitabu tunachomwomba Mungu atufunulie, hicho ni Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo.

³⁸ Kitabu hiki kiliandikwa yapata A.D. 96, kulingana na waandishi, na ilikuwa ni mpendwa Yohana.

³⁹ Naye alikuwa na ono hili kwenye kisiwa cha Patmo, kisiwa kwenye Bahari ya Asia, yapata maili kumi na tano, ama kitu kama hicho, kukizunguka, katika mzingo, mahali penye miamba sana na palipojaa nyoka, na kadhalika. Ambapo, taifa la Kirumi lilikitumia kama Alcatraz, kama tungalipaita leo, mahali pa kuwahamishia wahalifu ambao serikali isingaliweza kuwazuia.

⁴⁰ Nacho Kitabu hiki kiliandikwa na mtume wa mwisho wa Bwana wetu Yesu Kristo, anayesadikiwa kuwa ni yule mpendwa aliyeegemea kifuani Mwake baada ya kufufuka; Naye akasema, “Inakupasaje wewe kama akikaa hata nijapo?” Yohana alikufa, mzee. Kila mmoja wa wafia imani alitia mhuri ushuhuda wao kwa damu yao wenyewe.

⁴¹ Yohana, mwisho wake ulikuwa hivi. Yeye alishikwa, kisha akachemshwa katika pipa kubwa la mafuta kwa masaa ishirini na manne, kwenye mafuta yenye moto yanayochemka, na wala hayakumdhuru hata kidogo. Nao wakamweka kule kisiwani, kama inavyoaminiwa na watu wote, kama mchawi, “Yeye aliyaloga mafuta ili kwamba yasimchome,” wao walisema. Bila shaka, ilikuwa ni Nguvu za Mungu, hizo. Huwezi kumchemsha Roho Mtakatifu amtoke mtu. Mbona! Kwa hiyo wao wakajaribu kumchemsha Yeye amtoke, bali Mungu asingeruhusu jambo hilo. Naye alikuwa na kazi atakayofanya. Basi mpaka Mungu amemaliza na mtu Wake, hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kumsumbua. Hivyo tu.

⁴² Sasa, Yohana akiwa mzee, yeye...wao wanaambiwa na wanahistoria, ya kwamba aliletwa ka—kanisani, kuhubiri. Naye alikuwa mzee sana, jambo pekee ambalo angesema, lilikuwa, “Enyi watoto wadogo, pendaneni.”

⁴³ Nawaambia, hilo ni jambo zuri sana la kuhubiria. “Watoto wadogo, pendaneni.” Kadiri ninavyokuwa mzee, katika huduma sasa, na ninii yangu...karibu katika mwaka wangu wa ishirini na moja. Nafikiri, wakati wote ninaposonga mbele, kwamba jambo hili...Kadiri ninavyofikiri habari za Bwana Yesu, ndivyo ninavyoanza kuona kwamba upendo ndio unaofunika jambo hilo lote. “Pendo la Mungu, limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu.”

44 Sasa tutasoma tu aya chache hapa, kusudi tuanze, kisha tutaingia moja kwa moja katika fundisho la kanisa. Kisha tujaribu kulileta mahali, Mungu akipenda, katika kiasi cha wakati huu nilio nao, kulileta mahali ambapo tunaweza kufikia mahali ambapo tunaweza kuingilia, *Alama Ya Mnyama*, kwa ajili ya kesho usiku.

45 Sasa jambo hili ni kwa ajili ya kanisa. Sasa nitajaribu kupata, kwa vyo vyote, kanisa la Efeso, kanisa la kwanza, na kanisa la mwisho tunaloishi sasa, kanisa la Laodikia sasa.

Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika na kumwonyesha. . . akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana;

46 Sasa, Maandiko yanatupa mahali pa kuanzia hapa. Ni, “Ufunuo. . .” Ama, neno *Ufunuo* linamaanisha “kitu ambacho kimefunuliwa,” “Ufunuo wa Yesu Kristo,” aliopewa Yohana. Na malaika alitumwa kushuhudia, ama kuonyesha jambo hilo.

Na aliyeshuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote yale aliyoyaona.

Heri asomaye. . .

47 Ni wangapi wangetaka kupata baraka? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, kisome! Mnaona, “asomaye.”

Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.

48 Kwa maneno mengine, si wakati u karibu wakati huo, lakini, “Wakati u karibu, wakati watakapoliona Neno hili likitimizwa, wakati wa ule Ufunuo mkamilifu.”

49 Wakati Mungu alipoanza, kama mwana sanaa anayechora picha ya kitu fulani, Yeye akianza kujaza sehemu zake. Unaweza kuanza kuona kitu hicho kikiumbika. Basi hapo unapoanza kwenye mwanzo wa Kitabu cha Ufunuo, unamwona Yesu Kristo akianza kuingia kwenye picha. Na kwenye mwisho Wake, unamwona Yeye akiwa mkamilifu, ameketi pamoja na Kanisa Lake, ametukuzwa; siku zote za dhambi na shida na majaribio zimekwisha, naye Kristo ameketi pamoja na Kanisa Lake, kwenye Mbingu kuu juu.

50 Vema, aya ya 4. Sikilizeni. “Yohana kwa yale makanisa. . .” Sasa huyu ni Yohana akizungumza. Kwanza, ilikuwa ni Mungu akijulisha ule Ufunuo wa Yesu Kristo. Pili:

Yohana, kwa yale makanisa. . . yaliyoko Asia: Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja; na zitokazo kwa roho saba walioko mbele za Mungu;

51 Loo, laiti tungalikuwa tu na ubao hapa sasa, kuchora, kidogo, mnaona, “Roho saba zilizoko mbele za Mungu.”

52 Sasa kuokoa muda kidogo, na tukiamini ya kwamba mimi . . . nikijua ya kwamba nisingenukuu vibaya jambo lo lote, kwa cho chote kile ulimwenguni. Basi mkiona tashwishi ndogo juu yake, liandikeni kisha mkaniulize mimi, nami nitawapa Andiko lake. Basi sasa kwa kuwa hatuna budi kuharakisha tupate kuingia katika jambo hili, kuokoa wakati.

53 Sasa, “Roho saba walioko mbele za Mungu.” Hizi Roho saba ziliwakilishwa kama Roho saba ambazo zingetumwa kwa ajili ya Nyakati Saba za Kanisa, “Roho saba walioko mbele za Mungu.” Tungechukua kutoka katika Agano la Kale, na kuchukua kutoka pale, kama tu tungalikuwa na wakati.

Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha . . .

54 Jamani, mwangalie tu Yohana akimalizia yote kabisa pale, wakati alipoangalia. Anaendelea tu kuzungumza. Akasema:

. . . Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,

Na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu . . . Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina.

55 “Ametufanya kuwa makuhani na wafalme kwa Mungu.” “Kutufanya” ni wingi. Si “kunifanya mimi kuhani na mfalme;” lakini, “kutufanya,” Kanisa.

56 Sasa yeye anayaambia makanisa haya saba, kwa kuwa ni Nyakati Saba za Kanisa.

57 Sasa yeye alisema, “Ukuu na utukufu, na uwe Naye milele na milele.”

58 “Ametufanya makuhani.” Mlipata kujua kuhani ni nini, afisi yake ni nini? Kuhani anapaswa kutoa sadaka, na uombezi. Na katika Waebrania . . . Ilisema ya kwamba sisi, Kanisa, ni ukuhani mtakatifu, “Ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa kipekee.” Mnaona? “Taifa takatifu, watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme.” “Kutoa,” hili hapa sasa, “kutoa dhambi za roho,” kila mwanamume na mwanamke anayemjia Mungu anaingia katika lile pazia.

59 Katika Agano la Kale, kulikuwa tu na . . . Kulikuweko na pazia lililoning’inia kati ya mahali patakatifu na Patakatifu pa patakatifu. Ni Haruni tu, peke yake, aliyepaswa kuingia mle, mara moja kwa mwaka. Bali kila mtu aliyefanyika kuhani, angalikula, ama kuonja ile mana ya asili ambayo Musa na Haruni waliokota siku ya kwanza mana ilipoanza kuanguka kutoka Mbinguni. Wakati walipovuka mto wa Yordani . . .

⁶⁰ Adui waliuawa, nyuma yao. Kisha siku iliyofuata wakatoka, na kila mahali ardhini, kulikuweco na mikate midogo. Mungu alimwaga kutoka Mbinguni. Waliita “mana,” ilikuwa na ladha ya asali. Nao watu walipaswa kuokota tu ya kutosha kwa siku hiyo moja. Kama waliweka akiba, ilioza.

⁶¹ Na Mungu aliwaambia Musa na Haruni waondoke waende wakaokote pishi zake kadha, vikapu vikubwa, na kuvipeleka kwenye . . . karibu na lile sanduku, Mahali Patakatifu.

⁶² Ndipo pale, kwamba, kila wakati baada ya kizazi hicho, ambacho . . . Kila kizazi kilichofuata hicho, kadiri tu ukuhani huo wa Kilawi utakavyodumu, nafikiri. Na kila mtu aliyestahili kuwa kuhani, alipochaguliwa kuwa kuhani, yeye alikuwa na haki kamilifu ya kupokea mego moja ya ile mana ya asili. Wazieni jambo hilo. Ni majaliwa ya namna gani ambayo hao watu walifikiri wangukuwa nayo, wakati mtu alipojua ya kwamba anaingia kwenye ukuhani! Yeye alikuwa anaenda kupata me—mego moja ya chakula cha kimbinguni kilichookwa kimbinguni, kilichokorogwa kimbinguni, ambacho kilitoka mbinguni kwa Mungu, kilichokuwa kimehifadhiwa kimbinguni.

⁶³ Huduma yote ni ya kimbinguni. Watu wanawezaje kusema ya kwamba wao ni Wakristo, na kukana ya kimbinguni? Sijui jinsi wanavyofanya jambo hilo, mimi mwenyewe. Angalia. Jinsi lilivyo la kimbinguni! Yeye alipata mego ya kimbinguni, mara alipofanyika kuhani.

⁶⁴ Ni mfano mzuri jinsi gani sasa, ya kwamba kila mtu . . . Siku hizo, walipaswa kuzaliwa katika ukoo fulani, Mlawi, kabla ya kuwa kuhani, lakini sasa ni “atakaye, na aje.” Mnaona? Na mara walipokuja, hata hivyo, wao walipaswa . . . Uzazi unahesabiwa mle, pia. “Huna budi kuzaliwa mara ya pili.” Na kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa mara ya pili, kwa Roho wa Mungu, ana haki ya (siku hizi) ile mana. Mana hii ni Roho Mtakatifu.

⁶⁵ Wakati Petro . . . baada ya kutoka katika ule mchafuko mkuu, na uoga ulikuwa umewatoka, na Bwana alikuwa anawabariki, kisha Roho Mtakatifu akashuka kwenye Siku ya Pentekoste. Wao walitoka wakaenda mitaani wakaanza kupiga makelele, na kutenda kama watu wenye kichaa, kiasi kwamba watu wote walidhani kwamba wamelewa pombe. “Aisee, sijui tutakalofanya juu ya jambo hilo?” Kila m- . . . Hata ulimwengu wa kidini, wakati huo, ulidhani watu hao wamelewa.

⁶⁶ Basi sikiliza, rafiki yangu Mkatoliki, Bikira Mariamu aliyebarikiwa alikuwa pamoja nao. Basi iwapo hangeweza kuingia Mbinguni mpaka alipokwenda kule juu na kuonja Kitu kilichomfanya atende kama mwanamke aliyelewa, utaingiaje kule na kitu cho chote ila hicho? Mnaona? Bali yeye alipokea Kitu Fulani. “Mia moja na ishirini, pamoja na wale wanawake, Mariamu Magdalene na hao wengine,” nao

wakatoka wakaenda mitaani, wakitenda kama watu waliolewa, wakiopesukapepesuka. Mpaka, ninii halisi . . .

⁶⁷ Kama mtaruhusu hili tamshi; kanisa erevu la siku hizo lilisema, “Waangalieni! Hilo linaonyesha wao ni kitu gani. Wote wamejaa divai mpya.”

⁶⁸ Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Sasa sikilizeni, Petro alisema . . . Kisha wakaanza kusema, kasema, “Enyi watu wa Yerusalemu, ninyi mkaao Yeru- . . . Yuda, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. Watu hawa hawakulewa.” Sasa ninazungumza juu ya kanisa la Waefeso hapa sasa. Mnaona? Mnaona? Sawa, wakati wa kwanza wa kanisa. Yeye alisema, “Sivyo mnavyodhania, watu hawa hawakulewa. Hii ni saa tatu asubuhi; baa hazijafunguliwa bado. Mbona, hii ni saa tatu ya asubuhi.” Akasema, “Lakini Jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli. Limeandikwa katika Biblia yenu wenyewe, kwenye Biblia yenu wenyewe, hili limeandikwa, ya kwamba jambo hili litatukia. Mbona,” kasema, “iliwapasa kujua jambo hili, enyi waalimu.”

⁶⁹ Vema, yawezekana, kama vile tu—kama vile tu kanisa lilivyoingizwa chini ya dhihirisho hilo, na dhihirisho lilo hilo liliahidiwa kwa ajili ya siku za mwisho, hivi hamwezi kuelekeza kule nyuma na kusema, “Hili ndilo lililonenwa?” [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo. Nao ulimwengu wa nje haujui kitu juu ya jambo hilo; Hilo, Hilo ni upuuzi kwao. Basi wao walisema . . .

⁷⁰ Alisema, “Angalieni hapa.” Nao wakasema sasa, waliposikia jambo hili . . . Akawaambia jinsi walivyokuwa wamemsulubisha Yesu. Na kila wakati . . .

⁷¹ Unaweza kusamehewa kwa kumsulubisha Yesu. Unaweza kusamehewa kwa kuapa bure kwa Jina Lake bure. “Bali kila anayenena dhidi ya Royo Mtakatifu hatasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu ama ulimwengu ujao.” Tuko katika siku za mwisho, kwa hiyo iweni waangalifu. Tembeeni kwa unyenyekevu. Iweni na roho iliyovunjika na kupondeka; moyo mnyenyekevu, ulio tayari kumwacha Roho Mtakatifu awaongoze. Amina. Sawa. Loo, jamani!

⁷² Hawa hapa, wote wako kule, watu tu wakitenda kama . . . Wao walikuwa waoga, masaa machache hapo awali; wamejifungia katika chumba cha juu. Lakini wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu yao na kuijaza mioyo yao, wakatoka wakaenda barabarani! Sidhani wao walikuwa- . . . Wao hawakuwa wanafanya mambo mabaya. Wao walikuwa kule nje wakifurahi na kumsifu Mungu, na—na kwa njia fulani hivi kwamba kulikuwa na dhihirisho. Wao hawakuwa kule nje wakizozana tu mmoja kwa mwingine sasa, au walikuwa Methodist au Batisti, wao walikuwa . . . kama walikuwa Mafarisayo au Masadukayo. Walikuwa kule nje wakifurahi kwa

sababu wameonja utamu wa Mbinguni katika nafsi yao. Mungu alikuwa amewapa mana ya rohani.

⁷³ Sasa, kama vile Mungu alivyomwaga mana kule katika hali ya kawaida, nayo ikadumu mradi wao walikuwa safarini; mfano mzuri. Na katika ile siku waliyoingia kwenye nchi ya ahadi, ile mana ikakoma.

Na kwenye Siku ya Pentekoste, jambo lile lile. . .

⁷⁴ Angalia pentekoste, kwa Musa. Waliangalia nyuma wakaona adui amekufa. Miriamu akanyakua tari, akaanza kuicheza, na kupiga makelele, na kucheza, na kukimbia huko na huko ufuoni. Hao wanawake wakamfuata, wakifanya jambo lile lile. Kisha Musa akainua mikono yake, akaimba katika Roho.

⁷⁵ Kwenye Pentekoste, hao wanawake wakatoka, wakipepesuka, na kuruka, na kucheza, na kupiga makelele. Petro akasimama katikati yao, na kusema, “Enyi watu wa Yuda, nanyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkayasikie maneno yangu. Kwa kuwa hawa si walevi, kama mnavyodhanja, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, wana wenu na binti zenu watatabiri; juu ya wajakazi Wangu, na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu; nao watatabiri. Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na katika nchi chini; nguzo za moto, mvuke, na moshi. Ndipo itakuwa, kabla haijaja siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, kwamba kila atakayeliita Jina la Bwana ataokolewa.’” Akazidi kuendelea mbele, akihubiri.

⁷⁶ Basi waliposikia jambo hili, walisikiliza. Kasema, “Hebu mwangalieni jamaa yule! Alipata wapi elimu hii?” Baadhi yao wakasema, “Yeye hawezi hata kuandika jina lake mwenyewe.” Biblia ilisema, “Yeye alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa. Ametoka kwenye shule gani? Hakuna. Vema, jambo hili lilitokea jinsi gani? Jambo hili lilitukia jinsi gani?” Wao walitambua, wakasema, “Vema, aisee, mtu yule kweli anayanukuu Maandiko. Nasi kamwe hatukusikia Jambo hilo jinsi hiyo hapo awali.” Mnaona?

⁷⁷ Akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpatae ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, watoto wenu, kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Kwa maneno mengine, “Baraka hii ya mana iliyoshuka hapa, kama ile mana ilivyofanya kule nyuma, itakuwa kwa ajili ya kizazi hiki, kizazi kifuatacho, kizazi kifuatacho, kwa Jeffersonville, Indiana, na hata pande za mwisho za ulimwengu.”

⁷⁸ Na Roho Mtakatifu yule yule aliyeshuka wakati huo, anashuka sasa; matokeo yale yale, jambo lile lile, watu wale wale. Mnaona ninalomaanisha? Kamilifu tu!

⁷⁹ Angalia, “Nitampa; yeye ashindaye, nitampa Mkate wa Uzima.” Yeye alisema jambo hilo mbele ya moja ya yale makanisa. “Naye hataona kiu tena, wala hataona njaa tena. Hataona kiu tena.” Kama mtu akiwahi wakati mmoja... Hili hapa; jiandaeni mwe tayari. Kama siku moja mwanamume ama mwanamke akipata kwa kweli kumpokea Roho Mtakatifu, hutaweza kamwe kumtikisa tena. Yeye anajua mahali alipo. Unaweza kuja na itikadi na kila kitu. Yeye atatembea moja kwa moja kupitia kwenye hizo. “Hataona kamwe kiu tena.” Yeye anajua kabisa Mwenye Kumfanya ni Nani; hatachanganyikiwa kamwe. Haimsumbui; anasonga mbele moja kwa moja.

⁸⁰ “Nitampa Chakula cha Uzima, naye hataona njaa tena, wala hataona kiu tena.” Mnaona? “Na Mti ulioko katikati ya bustani ya Mungu, naye atakula kwake, mnaona, ule Mti.” Ambao, ule Mti ulikuwa ni Yesu Kristo. Mnaona? Naye Kristo Yesu, akiwa amekufa, alirudi katika mfano wa Roho Mtakatifu, kwa hiyo Yeye yuko hapa, na ndiye mana inayoliwa Kanisani.

Angalia, tazama, hiyo, aya ya 6.

Na kutufanya kuwa makuhani, na wafalme kwa Mungu,...

⁸¹ “Ukuhani wa rohani; taifa la kifalme; dhabihu ya rohani.” Ni kitu gani sasa? “Dhabihu za kiroho, hiyo ni kusema,” tukiyanyukuu Maandiko, “hiyo ni kusema, matunda ya vinywa vyetu, tukilisifu Jina Lake.” Sasa ni kitu gani cha namna gani? “Dhabihu ya rohani.”

⁸² Sasa, sasa afadhali tuanze papa hapa, angalia, mahali pazuri pa kuanzia.

⁸³ Wakati mchafuko mdogo unapokuja kanisani, hukimbii sasa upande mmoja na kubenua midomo sasa. Kama ukiibenua, bila shaka wewe si kuhani. Unaona, unaomba mpaka uridhike. “Dhabihu ya rohani, matunda ya midomo yetu tukilisifu Jina Lake.” Mnaona ninalomaanisha?

⁸⁴ “Vema,” unasema, “Kweli sijisikii kutoka kwenda kanisani.” Lakini wewe ni kuhani. Ni wajibu wako. Huna budi kuwa kule.

⁸⁵ “Vema, sijisikii kutaka kushiriki katika ibada.” Wewe ni kuhani, “ukitoa dhabihu, dhabihu ya rohani.” Si kumpa mtu fulani kitu fulani cha nipe-nipe, kama wanavyokiita siku hizi; hayo yote ni mema, sina kitu dhidi yake. Si kwenda kumfanya mtu fulani aje kanisani; hayo yote ni sawa, sina neno dhidi yake. Lakini, ni wewe, *wewe* kutoa dhabihu ya rohani, “matunda ya midomo *yako* ukilisifu Jina Lake.”

⁸⁶ Utakapoorika wakati ukija ambapo kila mtu anakufuru na kusema mambo vibaya, na kufanya mambo mabaya, utafanya nini, utaondoka? Unapaswa kusimama pale ukiwa na dhabihu ya rohani, ukisema, “Damu ya Yesu inasafisha dhambi zote,” inanifanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu.”

“Una kichaa, ewe jamaa!”

⁸⁷ “Kulingana na yale unayosema. Ni sawa. Lakini, kwangu mimi, ‘Ni Uweza wa Mungu uleta wokovu.’ Ninaamini Jambo hilo.” Mnaona?

⁸⁸ Sasa, unasema unaamini katika kuponya Kiungu? “Loo, aha, siamini. . . Afadhali nimwulize mchungaji wetu.”

⁸⁹ *Wewe* unaonaje juu ya jambo hilo? Wewe ni kuhani sasa. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara mbili—Mh.] Wewe ndiwe jamaa huyo. Sema, “Naam, bwana! Ninaamini jambo Hilo, kwa maana Neno la Mungu linasema ndivyo ilivyo!” Unaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu? “Ndio, bwana!” Unajuaje? “Nimeupokea Huo.” Amina. Baraka ya rohani! Roho Mtakatifu aliyeshuka juu ya wale mitume, Roho Mtakatifu yeye yule hushuka sasa.

⁹⁰ Unasema, “Kwa hao mitume tu”? Tutatatua jambo hilo katika muda kidogo, tuone kama ilikuwa hivyo ama la.

⁹¹ Vema, “Ukuhani wa rohani, tukitoa dhabihu za rohani.”

Sasa, sasa aya ya 8 ya . . . ya 7.

Tazama, yuaja na mawingu; . . .

⁹² Sasa hebu nisimame hapa kwa muda kidogo. “Mawingu,” haimaanishi ya kwamba yeye anakuja kwenye wingu kubwa la ngurumo.

⁹³ Na, mama, namtakia heri, yeye ameketi hapa mahali fulani. Nilipokuwa mvulana mdogo, alikuwa akiketi na kuniambia, kasema, “Yeye yuaja juu ya mawingu makubwa; tutafufuka siku moja, na Mungu atakuja.

⁹⁴ Na, sasa, “mawingu” ambayo anakuja kwayo. Kama tungalikuwa na wakati kuyarudisha haya yote nyuma, na kupata msingi halisi wa jambo lote zima! Sasa, “wingu” analokuja nalo, si wingu kama la ngurumo. Bali, ni “wingu la utukufu,” analokuja nalo. Mnaona? Mnaona?

⁹⁵ Sasa, hapo Yesu alipofunikwa kwa wingu na Mungu, juu ya Mlima wa Kugeuzwa, “mawingu yalimfunika pamoja na vazi Lake.” Mnaona?

⁹⁶ Na wakati Eliya aliposhuka, wingu lilishuka likamchukua juu. Si—si Mwali wa Moto, si. . . Ninamaanisha, si wingu la ngurumo, bali, “wingu la utukufu.”

⁹⁷ Uwepo Wake mkuu wenye utukufu utaigusa dunia. “Yuaja na mawingu.” Loo, napenda jambo hilo! “Mawingu,” kutakuwa na wimbi baada ya wimbi, la utukufu Wake, utakaokuja kila mahali duniani, ndipo ufufuo wa watakatifu utakuja. Wakati yule Roho Mtakatifu mbarikiwa ambaye ameishi miyoni mwao, nao wakafa, na mizoga yao imelala kule, na madoa ya majonzi mashavuni mwao, na mambo kama hayo, nao wamewekwa hapa

nje makaburini. Wimbi kubwa la Roho yule yule, na “whoossh,” wimbi baada ya wimbi!

⁹⁸ “Yeye aliyekuwa wa mwisho atakuwa wa kwanza, naye aliyekuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho.” Inawezaje kuwa namna hiyo? Huo ndio utaratibu wa ufufuo. Mimi sitamjua mtu ye yote katika kizazi kilichonitangulia, wala kizazi kitakachonifuata. Nitawajua wale walio katika kizazi hiki. Na kila kizazi kitakuja, kimoja baada ya kingine, jinsi tu kilivyoingia ardhini. “Hao waliokuwa wa mwisho watakuwa wa kwanza.” Hakika, haina budi kuwa namna hiyo. Mnaona? Nitawajua watu wangu. Jamaa anayefuata, babangu, atawajua watu wake; babu yake, watu wake; na moja kwa moja kwenda chini namna hiyo.

⁹⁹ Wimbi baada ya wimbi, baada ya wimbi, baada ya wimbi, huku watakatifu wakifufuka kutoka kila mahali! Jambo hilo si litakuwa zuri sana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Amina. Hilo linawafanya wazee kujisikia vijana tena. Naam. Sasa angalia kwa makini. Vema.

...anakuja kwa—kwa *mawingu*; na kila *jicho litamwona*, (haidhuru walikufa zamani namna gani; wao wangali watamwona yeye), na *hao waliomchoma*; na *kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake*.
Naam. Amina.

¹⁰⁰ Ilimbidi Yohana kupiga makelele, “Amina!” Hiyo ni kusema, “Na iwe hivyo! Na iwe namna hiyo!”

Mimi ni Alfa na Omega, . . .

¹⁰¹ Sasa *Alfa* ni “A” katika alfabeti za Kiyunani. *Omega* ni “Z” katika alfabeti za Kiyunani. Sasa, kwa maneno mengine, kama ilifasiriwa leo, “Mimi ni A mpaka Z.” Sasa huyu ni nani tena? “Mimi ni wa Kwanza; Mimi ni wa Mwisho. Mimi ni kutoka A mpaka Z.”

¹⁰² Laiti tungalikuwa na wakati wa kuingia katika Uungu wa Kristo, sasa hivi, jambo ambalo lingekuwa muhimu sana wakati huu, Uungu.

¹⁰³ Kwa hiyo, siku ambazo kila mmoja anajaribu kumfanya Yeye mwalimu tu, mfalsafa tu, ama nabii tu. Yeye alikuwa Mungu. Aidha alikuwa Mungu ama mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu uliopata kuwa naye. Kama alikuwa nabii, damu Yake ilikuwa ya mwanadamu. Kama Yeye alikuwa mwa—mwalimu, mfunzi, damu Yake ilikuwa ya mwanadamu.

¹⁰⁴ Yeye alikuwa Mungu, na Damu Yake ilikuwa ya Kiungu. Mwenyezi Mungu alimtia uvuli bikira Mariamu na kuumba chembechembe ya Damu katika tumbo lake la uzazi ambayo ilimzaa Mwana, Kristo Yesu. Ndipo Mungu akajidhili na kuishi katika mwili huo, Mungu (Imanueli), aliyefanyika mwili kati yetu; kuondoa dhambi.

¹⁰⁵ Wakati Mungu alipomfanya mwanadamu Wake wa kwanza, Yeye alimfanya katika mfano Wake, ambaye alikuwa ni mtu wa rohoni, katika Mwanzo 1:26. Vema. Ndipo hapakuwepo na mtu wa kuilima ardhi, baada ya Yeye kumfanya mtu, mwanamume na mwanamke. Tutafikia jambo hilo, baada ya muda kidogo, juu ya zile “nyota saba.” Lakini tu... Lakini Yeye alimfanya mwanamume na mwanamke pia, kule nyuma katika mwanzo, hiyo ni kweli, “katika mfano Wake.” Naye Mungu ni Roho.

¹⁰⁶ Halafu, Mwanzo 2, hapakuwepo na mtu wa kuilima ardhi, kwa hiyo Mungu akamweka katika mwili; akamfanya mtu, si katika mfano Wake, bali kutoka katika mavumbi ya ardhi, hiyo ni kweli, akampa mkono kama wa kima, na mguu kama wa dubu, ama cho chote kile; sijui, bali Yeye alimpa hisi tano kwa kuwasiliana na makazi yake ya duniani. Kisha mtu huyo akafanya dhambi.

¹⁰⁷ Ndipo Mungu akashuka akafanyika mwanadamu, apate kuondoa dhambi ya mwanadamu, (amina) kukomboa!

Mimi ni Alfa na Omega, . . .

¹⁰⁸ Nilimtazama hapa katika Ufunuo sura ya 4. Wakati Yohana alipogeuka kuona Sauti hii tena, ile iliyokuwa ikinena naye, “Yeye alikuwa ameketi kwenye Kiti cha Enzi, na upinde wa mvua ukiwa juu ya kichwa Chake.” Na upinde wa mvua una rangi saba kamilifu, na hizi ninii saba kamilifu. . . rangi ziliwakilisha zile Nyakati Saba za Kanisa. Hiyo ni kweli, tena. Basi ilikuwa ni nini? Hili hapa. Ndugu, hili ni jipya. Angalia, rangi saba kamilifu, saba! Nao upinde wa mvua unawakilisha agano.

¹⁰⁹ Mungu alimpa Nuhu upinde wa mvua, kwanza, kama agano. Na vitu hivyo vingali duniani, kama ahadi ya Mungu mbele yake; wakati inaponyesha, yeye anaona ule upinde. Yeye alisema, “Sitaingamiza tena kwa mvua.”

¹¹⁰ Kisha alimwalia Yesu, alikuwa na rangi saba za upinde wa mvua juu Yake; Yeye alikuwa katika huu, ambao ulikuwa ni agano la Mungu. Naye alikuwa amesimama katikakati ya Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu. “Naye alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki.” Yaspi ilikuwa ni Reubeni, na jiwe la akiki lilikuwa ni Benyamini; hao walikuwa wa kwanza na wa mwisho wa wale wazee wetu. Hao “Alfa na Omega; Mwanzo na Mwisho,” na zile rangi saba za upinde wa mvua, zile Nyakati Saba za Kanisa, lile agano pamoja Naye, katika vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu, pamoja na zile nyota saba. Loo, ni picha ya namna gani, kama tukiifikia baada ya kitambo kidogo, labda, Bwana akipenda. Vema.

*. . . Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema
Bwana Mungu, aliyeko . . . aliyekuwako na atakayekuja,
Mwenyezi.*

111 Loo! Yeye ni nani? Ufunuo huu ni wa nani? Yesu Kristo. Pia, hapa, Yeye si nabii. Hapa, Yeye ni Mwenyezi, Mungu aliyedhihirishwa; Alfa, Omega. “Mimi ni kutoka A mpaka Z. Mimi ni Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja. Mimi ni Mwenyezi.” Ni dhahiri sana, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakuna nafasi ya mabishano hapo. “Bwana, Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja, Mwenyezi.”

112 Sasa Yohana anazungumza. Sikilizeni.

Mimi Yohana, ndugu yenu na mshiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kinachoitwa Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, . . .

113 Aisee, ungeweza kuwazia mtu akiwekwa katika mahali kama hapo, kwa ajili ya Neno la Mungu? Naam.

. . . kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo.

114 Yeye aliamishwa kule nje kwa ajili ya kuwahubiria Neno watu wa dini. Hivyo ndivyo Neno linavyosema. Sivyo? Yeye alikuwa huko nje akihubiri; amehamishwa, amefukuzwa kutoka kanisani, kutoka kwa watu, kutoka kwenye ulimwengu mzima. Amina. Bali yeye hakufukuzwa kutoka Kwake Yeye aliyempenda na kumwosha katika Damu Yake Mwenyewe. Yeye alikuwa pamoja na Uwepo Wake, katika kisiwa kiitwacho Patmo, “kwa ajili ya Neno la Mungu.”

115 Sijui ni wahubiri wangapi leo wangeenda? Ashuke chini mpaka aende afanye, kitu fulani kidogo, tunafadhaishwa na kitu kidogo, tunaudhishwa sana nacho. Na hapa mtu huyu alikuwa amechemshwa katika mafuta kwa masaa ishirini na manne, kisha akatupwa kwenye kisiwa cha Patmo, na Bwana alikuwa angali pamoja naye.

116 Ninaupenda tu ule wimbo wa zamani waliozoea kuimba, “Kama Yesu akiambatana nami, nitaenda po pote pale.” Tunauimba, bali sijui kama tunamaanisha jambo hilo kweli. Kwa unyofu wa moyo wangu, haitachukua muda mrefu sana hata utakapopewa nafasi kuthibitisha jambo hilo, kwa hiyo afadhali uwe na uhakika kabisa. Chunguza, fanya hesabu, uone kama kila kitu ni sawa kabisa.

117 Sasa, jinsi tu, sina budi kuanza hapa sasa. Yohana anajibu, naye akasema alikuwa “katika kisiwa cha Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda.”

Nalikuwa katika Roho, . . . (napenda jambo hilo.)

Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana . . .

118 Akinena juu ya siku nyingine, sasa; kwa marafiki zangu Wasabato, jambo ambalo bila shaka tutalifikia, baada ya kitambo kidogo. Vema.

...katika Roho, siku ya Bwana; aliingia katika Roho, nikasikia sauti kuu nyuma yangu,...sauti ya baragumu,

¹¹⁹ Hebu tusiiache mifano hii sasa. Tunaweka msingi sasa, ili kwamba tujue yale tunayozungumza habari zake ninapokuja hapa. Tuone kile tutakachonena habari zake, “Ni nani? Jamaa huyu ni nani? Ufunuo wa Yesu Kristo ni nini? Yeye ni Nani, hata hivyo? Ulikujaje? Una maana gani kwangu?” Angalia kama una maana yo yote kwako, unaona. “Angalia kinachotukia kule, kwangu.” Angalia.

Nalikuwa katika Roho...

¹²⁰ Haidhuru wewe ni mwema namna gani, u mtawa jinsi gani, u mhudumu ama mfuasi wa kawaida vipi, na cho chote ulicho, hutaweza kufika mahali po pote na Mungu mpaka utakapoingia katika Roho. Hiyo ni kweli. Simaanishi kuingia katika mwamsho. Ninamaanisha kuingia katika Roho. Unaona? Unaona? Unaona, ukiingia katika mwamsho, unafanya jambo lo lote. Bali unapoingia katika Roho, unaona mambo. Hiyo ni kweli.

¹²¹ Naweza kumwazia mzee Eliya, yule nabii wa zamani, kule chini siku ile wakati—wakati ninii...wakati mwana wa Ahabu, hao, walipokuwa wamefanya mapatano na wasioamini, na—na Yehoshafati alikuwa amejunga nao. Nao wakatoka wakaenda jangwani kwa muda wa siku saba, nao hawakuchukua dira yo yote. Kwa siku saba tu, ya kutosha kuwashughulikia kwa muda wa siku saba; hawakumtaka shauri Bwana; walitoka tu wakaenda, kwa vyo vyote.

¹²² Je! hivyo si kama watu walivyo? “Loo, nitakwambia, hiyo ni kazi bora zaidi. Nitaliacha tu kanisa hili niende kwenye *lile*.” Sasa afadhali umtake shauri Bwana juu ya jambo hilo, uone ni nini.

¹²³ Katoka kaenda kule wakajikuta wao wameingia shidani. Maji yalikatika. Hiyo ndiyo shida ya makanisa leo, mnahangaika huku na huko mkifanya mambo mengi sana msiyomtaka Bwana shauri juu yake, na maji yenu yanakatwa. Mnashangaa kwa nini hampati baraka mlizokuwa mnapata, na nguvu za Mungu zikitenda kazi kati yenu, labda bomba la maji limekatwa. Mwajua, mnapokosa, maji...

¹²⁴ Ninaingia jangwani wakati mwingine, nje huko Arizona. Na naona ya kwamba kila kijiti cha siku nyingi kwenye hilo jangwa ni chenye kudhuru; kitakuchoma. Kila wakati unapokiingilia, kitakuchoma. Kwa kuwa hakina maji ya kutosha kukitunza, miiba inaota kwa ajili ya kujihami.

¹²⁵ Unarudi hapa, ama kule Oregon ama mahali fulani ambapo kunanyesha kila wakati, na kila kimoja cha hivyo vijiti vya namna ile ile hakina miiba. Mnaona, maji yanakifanya kiwe chororo.

¹²⁶ Basi hiyo ndiyo shida ya kanisa. Unapokauka kabisa na umefungwa, na kila kitu, unakuwa na baridi sana na wa kawaida na asiyejali, hupati baraka yo yote ya kiroho, ndipo moyo wako unajazwa kabisa na umejaa uchungu na hasira, na, kila mtu, “Loo, yule mwanamume atanitambua. Yule mwanamke atanitambua. Nitaliacha kanisa.” Ni kundi tu la miiba linaloishi jangwani. Hiyo ni kweli. Unachohitaji ni kunyeshewa Maji kidogo ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu, kulainisha huo moyo wa kale wa karata. Amina.

¹²⁷ Mimi si—mimi sijaribu kufanya mzaha. Ninajaribu kuwaelezea jambo hili. Ndugu, utakuja kuona, kama ukichukua ile alama ya mnyama, ni mahali gani utakaposimama. Nawe ni mdhaifu kabisa na huna tumaini kabisa utakapofanya jambo hilo. Hakuna msamaha kwake. Huwezi kamwe kujiondoa kwake. Hiyo ni kweli. Unaweza kufanya jambo hilo kwa kukonyeza jicho lako, karibu unaweza, unaona, kwa hiyo uwe mwangalifu. Sasa hili hapa. Utampa... Angalia, jangwa...

¹²⁸ Nilisema, ma—maji, jinsi vile maji yalivyoilainisha. Hivyo ndivyo tunavyofanya leo, kuingia katika Roho. Yohana alisema, “Nilikuwa katika Roho.”

¹²⁹ Wakati Eliya huko nje jangwani, wao walishuka. Yehoshafati akasema, “Na tushuke tukamtake shauri nabii.” Wao walishuka wakaenda mbele ya nabii.

¹³⁰ Vema, sasa, alitoa hasira yake yenye haki. Anamtazama jamaa huyo, basi akasema, “Mbona usimwendee mungu wa mama yako? Mbona usirudi kwenye kanisa lako la zamani, lenye baridi na la kawaida? Mbona ulinijia, wakati ulipoingia shidani?” Hilo halikuwa jambo zuri sana la kusema, bali kwa kifupi hilo ndilo neno alilomaanisha. “Mbona mkanijia mimi? Mbona hamwendi kwa mungu wa mama yenu? Ninyi nyote mna makanisa hayo makubwa na mazuri, na hao makuhani wote waliolishwa vizuri, na kadhalika, kule nyuma. Rudini mkawaulize jambo hilo. Mbona mnashuka mnanijia hapa?” Whiu! Jamani! Yeye kwa namna fulani alijigamba sana, kweli kabisa, siyoy? Akasema, “Kama siyo kwamba niliheshimu uwepo wa mtu huyo mtauwa, Yehoshafati; hata nisingalikuangalia.” Loo, jamani, huyo nabii aliingia katika hali ilioje! Sasa yeye yuko kabisa katika tatizo la namna hiyo.

¹³¹ Akasema, “Vema, niletee mpiga kinanda.” Watu wengine hawaamini katika muziki kanisani. Lakini yeye alisema, “Nileteeni mpiga kinanda.” Ikawa hapo mpiga kinanda alipoanza kupiga wimbo fulani mzuri wa kale, *Karibu Na Wewe, Mungu Wangu*; cho chote unachotaka kuuita, sijui mimi. Ikawa mpiga kinanda alipoanza, kuomba, Roho wa Mungu akamwingia yule nabii. Ikawa Roho alipomwingia, akaingia katika ono; akaanza kuona mambo.

132 Huna budi kupata Roho wa Mungu. Ama, unasema, “Siwezi kufahamu jinsi watu wanavyoweza kusema, ‘Amina.’” Ingia katika Roho siku moja. Hiyo ni kweli.

133 Siwezi kuona jinsi wao wanasimama kwenye mchezo wa mpira wa baseball na kupigana mgongoni na kupiga makelele na mayowe, na kutoa kofia na kushangilia. Inaonekana kama wenda wazimu kwangu mimi. “Vema,” unasema, “wewe si shabiki mzuri wa mpira wa baseball.” Mimi ni ninii tu.

134 Na wewe je, kama Mkristo? Vema. Hiyo ni kweli. Huna budi kuingia katika Roho wa jambo hilo.

135 Hivyo ndivyo ilivyo ulipokuwa unaenda kucheza dansi. Siamini ungeenda huko sasa. Hakika huwezi. Lakini kama uli—ulizoea kwenda, iliwabidi kucheza muziki wa mpira wa kibao, na kupiga bendi na kupiga ngoma, na kufanya kila namna ya kitu kilichoko juu ya jambo hilo; nao wanawake wanafurika kule, nusu uchi na kila kitu, na kucheza dansi sakafuni, na kadhalika; unaingia katika roho wa kucheza dansi. Vema, hiyo ni kweli, unaingia katika roho wa jambo hilo. Ni roho wa Ibilisi. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nafurahi mlisema, “Amina,” kwa maana ni kweli. Nitalithibitisha jambo hilo kwa Biblia. Hiyo ni kweli. Vema.

136 Wasema, “Vema, siamini jambo hilo, ndugu.” Vema, wewe, si yale unayosema, wala ninayowazia.

137 Ni yale Neno la Mungu lisemayo. Hilo ndilo linalomaliza kila kitu. Hilo ndilo Neno la mwisho. Naam, bwana. Yeye alisema, “Ukiipenda dunia, ama mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Hiyo ni kweli. Pia kumbuka maskini mwanamke yule wa zamani alimfundisha bintiye kucheza dansi ya kuruka-ruka, na vitu kama hivyo, kisha akashuka akaenda kule akacheza mbele ya mfalme, ndipo akadai kichwa cha Yohana Mbatizaji; watoto wake sabini walikufa kama makahaba na kwenye mti wa kunyongea. Unaweza kuona jinsi inavyofanya namna hiyo.

138 Mama wa Musa alikaa nyumbani, na akamweka, na kumfundisha Neno la Bwana, unaona kile kilichompata yeye na walio wake. Kupitia kwake akatokea . . . Ibrahimu, na kadhalika, na kuendelea moja kwa moja.

139 Sawa, inategemea tu na kile unachotaka kufanya. Wewe, wewe ni mtu mwenye hiari. Unatenda kile unachotaka kutenda. Sawa. Mungu ameweka mbele ya mwanadamu, kama vile katika bustani ya Edeni, Mti wa Uzima ama mti wa mauti. Unajichagulia mwenyewe. Mnaona? Cho chote nafsi yako inachotamani, hicho ndicho utakachokula. Angalia sasa. Nao walikuwa . . .

140 Nataka kusoma hili tena sasa. Yeye alikuwa katika Roho. Roho akaja juu yake. Akaanza kuona mambo. Sasa angalia.

Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia . . .

*Niliingia katika Roho, siku ya Bwana, nikasikia sauti
kuu nyuma yangu, . . . ya baragumu,*

141 “Baragumu.” *Baragumu* ni “tangazo.” Gabrieli, katika kule Kuja kwa Bwana, atapiga baragumu ya Mungu. Hii ilikuwa baragumu ya Mungu ikilia. Kwa maneno mengine, Yeye anajiandaa kutangaza kikomo cha Milele cha ulimwengu. Baragumu! Ni nini? “Jitayarishe. Nitakupa ufunuo wa Yesu Kristo, upate kuutoa kwa kanisa. Nitanena nawe, kile kitakachokuwa kikomo cha ulimwengu, kwa wale watakaopokea na wale watakaokataa.”

142 Baragumu ya Mungu. “Sikilizeni!” Kila mtu, wakati tarumbeta inapolia, hunyakua upanga wake na kusimama mahali panapofaa, anasimama sawasawa. Baragumu!

143 Paulo alisema, “Kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?”

144 Hivyo ndivyo ilivyo leo. Loo, ndugu, ninapoangalia kila mahali na kuona makanisa haya yote baridi, ya kawaida, na yasiyojali, na vitu kama hivyo, “wakiwa na mfano wa utauwa, na kukana Nguvu zake,” mtu anawezaje kujifanya tayari? Kutoa sauti isiyojulikana!

145 Wasema, “Vema, sasa, nitajiunga na makanisa. Nitaenda kule nikajaribu Methodisti, ama Batisti, ama la Kiluteri, ama la Kipentekoste. Nitafanya kitu fulani. Nitachukua hatua fulani.” Loo, siyo hivyo.

146 “Mtu asipozaliwa mara ya pili.” Sijali kama yeye ni Mmethodisti, Mbatisti, Mpentekoste, ama cho chote alichu, huna budi kuzaliwa mara ya pili; hutaingia kwenye ule Ufalme. Amina.

147 Angalia, “Sauti ya baragumu, ikiniambia, ‘Mimi ni Alfa na Omega.’”

148 Jambo la kwanza sasa, Yeye anajulisha hapa, “Mimi Niko, wa Kwanza na wa Mwisho.” Jambo la kwanza, wakati baragumu ya Mungu ilipolia, yeye aligeuka. Kisha akasema, “Mimi ni Alfa na Omega. Mimi ni tokea A mpaka Z. Mimi ni yote hayo sasa. Simama ukanisikilize, kwa kitambo kidogo.” Vema.

*. . . mwanzo na mwisho, . . . Haya uyaonayo uyaandike
katika chuo, . . . (hicho ni Kitabu hiki tunachosoma) . . .
ukayapeleke kwa hayo . . .*

149 Wapi? Kipelekwe kihalali. Wapi, kule nyuma kwenye ule wakati? La. “Kwa kanisa.” Kwa kanisa! Angalia.

*. . . Haya uyaonayo uyaandike katika chuo,
ukayapeleke kwa hayo makanisa saba yaliyo Asia: . . .*

150 Ambayo, yalikuwa mfano wa kanisa. Sasa tutafikia jambo hilo, katika dakika chache, tukionyesha jinsi Agano la Kale

lilivyoonyeshwa kwa mfano katika nyakati saba. Nyakati saba zilika, ama makanisa saba yalikuwa hapa Asia, ambayo Biblia inafundisha dhahiri, ambayo yalikuwa ni kivuli, ama mfano wa zile Nyakati Saba za Kanisa ambazo zilikuwa zinakuja. Na kwa msaada wa Mungu, na pamoja na Biblia, tunaweza kuthibitisha ya kwamba kila wakati wa kanisa ulikuwa hasa mahali ambapo Hiyo ilisema ungekuwa, mahali pale hasa ambapo Biblia ilisema ungekuwa. Nasi tuko katika mwisho wa wakati wa mwisho wa kanisa.

¹⁵¹ Na akarudi katika Agano la Kale, akachukua ile ndoto ya Danieli, na kumwonyesha lile ono la ufalme wa Kimataifa, jinsi alivyoona sanamu imesimama; yenye kichwa cha dhahabu, kifua cha fedha, na mapaja ya shaba, na nyayo na miguu ya chuma na udongo. Kisha akaonyesha jinsi kila moja ya hizo falme zilivyofuatana mmoja kwa mwingine, vile vile kabisa namna ile Biblia ilivyo sema. Pia, angalia, kichwa cha dhahabu, Babeli; Wamedi na Ajemi, Kiyunani; kisha himaya ya Kirumi; halafu himaya ya Kirumi ikavunjika-vunjika ikawa falme kumi, Rumi ya mashariki na ya magharibi, na kadhalika. Na mle ndani, kulikuweco na chuma na udongo, nazo hazingechanganyikana; Uprotestanti na Ukatoliki chini ya utawala ule ule wa Kimataifa. Naye alisema ya kwamba hata kujaribu kuvunja nguvu za mmoja kwa mwingine, wangeoana wao kwa wao, jinsi kabisa wanavyofanya leo, kabisa.

¹⁵² Na ufalme huo katika siku za wafalme hao. Mungu wa Mbinguni alikata jiwe kutoka mlimani, bila kazi ya mikono, ambalo liliipiga ile sanamu miguuni na kuzivunjilia mbali falme zote za Kimataifa. Ndipo Ufalme wa Kristo ukaongoza na kutawala, na kustawi, ukaifunika dunia na bahari na anga. Falme za Mataifa zikafifia kama pura, kama makapi katika sakafu ya kupuria kwenye majira ya kiangazi. Ni picha ya namna gani tunayoishi ndani yake! Hiyo ni kweli.

¹⁵³ Na leo, unaona Wakatoliki na Waprotestanti wakioana wao kwa wao, wakijaribu kuzivunja nguvu; unalea watoto wako, inakubidi kuahidi kuwalea wao namna *hii* au namna *ile*. Tutafikia jambo hilo, baada ya kitambo kidogo, katika siku chache usiku. Angalia jinsi ilivyo, na jinsi (ile nyingine) nguvu za chuma zilitawala hizo zingine, zikazivunja vipande-vipande na kuziharibu kabisa.

¹⁵⁴ Lakini Mwana-Kondoo akaja na kusimama! Nao watu watakatifu katika siku hiyo. . .

¹⁵⁵ Na jinsi ambavyo nguvu hizo za Kirumi zilipitia katika kila taifa. Hakuna nguvu zingine ulimwenguni, na kuna njia moja tu zinavyoweza kupita, ni kwa njia ya Ukatoliki, kanisa Katoliki, kuingia katika ulimwengu mzima, zikivunjavunja humo ndani. Ni picha kuu, ya ajabu sana hapa.

156 Sasa kwenu enyi Waprotestanti, msitoe viatu vyenu, maana, ndugu, mko moja kwa moja pamoja nalo. Nami naweza kuthibitisha jambo hilo kwa Neno la Mungu, mko moja kwa moja ndani yake sana kama tu—kama tu wengine wao.

157 Sasa, angalieni sasa, “Wa Kwanza na wa Mwisho. Unayoyaona, yaandike katika Chuo.” Basi Yeye alimwambia:

...uyaandike haya katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa... yaliyoko katika—katika Asia: Efeso, na Sardi, na Pergamo, ... na kadhalika, na Filadelfia, na Laodikia.

158 Sasa tutasimama hapo, kwa dakika moja ama mbili, tupate kuona nina wakati gani, kwa maana nataka kufikia jambo hili muhimu sana hapa, juu ya Waefeso, na kulivuta nilipeleke kwenye Laodikia, tuone kama hatulinganishwi na kanisa lile lile, mnaona, tuone kama hatuishi katika siku hii.

159 Loo, enyi Kanisa la Mungu aliye hai, amkeni mkaangaze. Angalieni. Hamtambui. Laiti ningalikuwa na namna fulani ya mshtuo ambao ningewapa, kwa njia fulani. Laiti Roho Mtakatifu angalikuja katika nguvu Zake kuu na kuwapeleka mahali ambapo mngeinyakua Biblia hii na kusema, “Hebu nilichunguze jambo Hili!” Mnapoona:

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara zilizotabiriwa na Biblia;
Siku za mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.” Hiyo
ni kweli.

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu zikiwa
zimetengenezwa na safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

160 Hiyo ni kweli. Loo, ni siku ya namna gani! “Uyaandike, ukayapeleke kwa hayo makanisa.”

161 Sasa, kama tu Israeli walivyokuja katika uzuri wao, nyuma huko mwanzoni chini ya Ibrahimu, wakashuka wakaja kupitia kwa wale wazee wetu. Na katika siku ya Ahabu likaingia katika nyakati za giza, wakati wa giza sana ambao kanisa liliwahi kuona. Likatoka kule nje... Basi katika wakati huo, jinsi ambavyo Ahabu alivyomwoa Yezebeli, akaleta ibada za sanamu katika lile kanisa lenye imani halisi.

162 Jambo lile lile, ambalo, Uprotestanti ulioa Urumi katika ile miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza, katika kanisa la Pergamo, kisha ukatoka ukiwa na ibada za sanamu, chini ya mfano wa Ukristo, ukaingia katika wakati wa uvuguvugu

unaokuja mbele zetu. Nasi tuko ndani yake sasa hivi. Tuko katika wakati wa uvuguvugu.

¹⁶³ Hamwamini jambo hilo? Sasa nitaketi chini kwenye . . . ninyi watu huko nje katika makanisa mengine. Mko katika wakati wa uvuguvugu. Nao wainjilisti wenu wanavuka dunia, kuizunguka dunia, wakihubiri mambo kama hayo; hamtafikia mahali po pote. Mnapiga makelele. . . Ninyi Wabatisti mnapiga makelele, “Milioni moja zaidi katika ‘44.” Mna nini mlipowapata? Mna kundi tu la wenye dhambi walioingia, wakijiandikisha majina yao kwenye kitabu, hiyo ni kweli, wanasema ni wafuasi wa kanisa la Kibatisti. Isitoshe, lakini, mna Wamethodisti, Wakampbeli, na hilo kundi lote, watu wa kawaida na wasiojali vile vile tu. Billy Graham alikuwa na jambo hilo, “Waongofu elfu thelathini,” akasema, “na majuma sita. . .” Na majuma sita baadaye asingepata thelathini. Kwa nini? Kwa nini? Wao hawakupata kitu, kwanza. Ni kundi tu la wenye dhambi, wanapoandika jina lao kwenye kitabu, chini ya mvuto wa ufufuo.

¹⁶⁴ Yeye alisema, “Ufalme wa Mungu ni kama mtu mmoja aliyetupa jarife baharini. Alipolivuta, alikuwa na kila kitu.” Alikuwa na ng’amba. Alikuwa na kamba. Alikuwa na kasa. Alikuwa na buibui. Alikuwa na wadudu wa majini. Alikuwa na nyoka. Hiyo ni kweli. Bali mle ndani, alikuwa na samaki wachache, pia.

¹⁶⁵ Na wakati mtu anapohubiri ufufuo chini ya nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu, jarife linavutwa likiwazunguka watu. Hiyo ni kweli. Na, walakini, kama mwanzoni yeye ni mdudu, yeye ni mdudu mwisho wa ufufuo.

¹⁶⁶ Kama yeye ni buibui wa majini, muda si muda, atazunguka akiangalia kila mahali, akisema, “Siamini upuuzi huu wa kale hata hivyo,” kisha aruke arudi majini.

¹⁶⁷ Kama yeye ni nyoka, atasema, “Nilikwambia jambo hilo,” kisha huyoo ataenda. Yeye alikuwa nyoka, kwanza. Asili yake ilikuwa nyoka. Naye hatakuwa kitu kingine mpaka asili hiyo itakapobadilishwa.

¹⁶⁸ Mtu hawezi kujiunga na kanisa, ama kupata mwamsho kabisa, ama cho chote kile, kisha awe Mkristo. Haina budi kuwa ni kuzaliwa kamili kwa Roho; akifa kweli, akilia sana, akilala pale hata awe mfu maradufu. Kumbukeni, uhai unaweza tu kutokana na mauti.

¹⁶⁹ Chembe ya mahindi, kama ikidumu, inadumu peke yake, haitamaanisha zaidi ya chembe hiyo moja ya mahindi. “Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, inakaa peke yake.” Bali inapoanguka pale, inaoza, inakuwa udongo, na kutoka katikati ya hali hiyo ya uharibifu inatokea chembechembe ya uhai inayoipa uhai na kuzaa nyingi zaidi.

¹⁷⁰ Kanisa lisipozaliwa mara ya pili, life kwa kanuni zake za imani na theolojia, na kadhalika, na kuzaliwa upya kwa Roho wa Mungu, litakuwa la kale, baridi, la kawaida, lisilomcha Mungu, lisilojali. Amina. Hiyo ni kweli. Hayo ni mahubiri ya mtindo wa kale na ya kifidhuli, bali yatakuokoa, ndugu. Hiyo ni kweli. Yatashikilia wakati tufani inapovuma vikali. Pata msingi imara. Ondoa uchafu wote kabla hujamwaga saruji yako; angalia, hiyo ni kweli, nayo nanga inashika chini vizuri na imekazika. Loo, ndugu, ni siku ya namna gani tunayoishi; wakati wa kanisa ulio wa kidehuri, usiojali! Naam, bwana.

“Kwa yale makanisa saba,” kasema, “tuma ujumbe huu.”

¹⁷¹ Sasa, katika huo wakati wa kanisa, wao walianza kuingia; waliolewa na ibada za sanamu. Wao wanafanya jambo lile lile sasa; wameingia, wakifanya jambo lile lile. Na kutokana na jambo hilo, ukaingia Ukristo wa kidehuri, wakaanza kufifia mpaka wao wanafikia wakati wa mwisho wa kanisa.

¹⁷² Sasa, kanisa la kisasa, ambalo tunaliita “madhehebu.” Sisi watu wa utakatifu, mwajua, tunawaita, “wa kisasa,” nao wanatoka nje kule na kuanza ufufuo wao, pia. Mnasema, “Hawafiki mahali po pote.”

¹⁷³ Lakini sasa ngoja kidogo tu. Tuna kitu gani? Hatuna kitu, si zaidi ya walicho nacho. Hiyo ni kweli kabisa. Mradi tu tunazozana na kuhangaika na kupiga makelele, tungali tunatembea kama mwanadamu; mpaka mtu anapoweza kushuka kwenda kwenye madhabahu na kuwa sawa na Mungu, mpaka anapoweza kutojali mambo madogo-madogo na kusonga mbele kama Mkristo apaswavyo kufanya. Chungu hakiwezi kuiita birika nyeusi. Kweli. Nanyi msiwakemee. Hebu na tusafishe hatua zetu kwanza.

¹⁷⁴ Mtuwile radhi, enyi wageni, ninalipa kanisa kofi kidogo la Injili sasa. Angalia, hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo mnayohitaji hasa.

¹⁷⁵ “Loo,” mnasema, “tumempata.” Kisha unaenda kule na kupiga piano kwa nguvu uwezavyo, na ngoma nyingi, na kukimbia huku na huko sakafuni, halafu unatoka unaenda na kuzozana na jirani yako. Umepata cho chote? A-ha. La, bwana. Kitu tu tulicho nacho ni uvuguvugu. Mradi tu muziki unacheza, tumechangamka. Muziki ukikoma, tunakoma. Ndugu, usimwite huyo jamaa mwingine kitu fulani; hebu na tuangalie mlangoni mwako wewe, kwanza. Amina.

¹⁷⁶ Nawaambieni, tunahitaji ufufuo wa mtindo wa kale kama tuliokuwa nao nchini, wakati wao walipolala kifudifudi usiku kucha. Si kufanya makelele, bali wakati huzuni halisi ya kiungu; na si kurudi kwenye madhabahu na kukaa, bali kutoka nje na kusahihisha mambo na jirani waliyekuwa wamekosana, na kusawazisha mambo. Mnajua hiyo ni kweli. Inachoma moto, lakini, ndugu, itakusaidia. Hiyo ni kweli. Huna budi kujua jambo hilo, rafiki yangu. Naam, bwana.

¹⁷⁷ Vuguvugu, hiyo ni hali ya kutisha sana kwa kanisa kuwemo. Msipojihadhari, Maskani ya Branham imeingia katika mkondo ule ule. Sikilizeni, mnajua mambo haya. Yamekwisha fundishwa, mwaka baada ya mwaka, mwaka baada ya mwaka, mwaka baada ya mwaka, kwenye jukwaa hili, yakiwaonya juu ya mambo haya yanayokuja. Ambapo, Biblia ilisema ungekuja wakati ambapo wangeenda kutoka mashariki hata magaharibi, na kaskazini na kusini, wakijaribu kulipata Neno la kweli la Mungu, nao washindwe kulipata. Afadhali utiwe nanga, mahali ambapo unajua unakosimama.

¹⁷⁸ Lakini wakati mtu amekwisha zaliwa mara ya pili; si mwamsho, si shauku fulani, si kwa kuandikisha jina lake kwenye kitabu cha kanisa, si kwa kujiunga na kanisa lililo kubwa sana jijini. Bali wakati kweli amelia vya kutosha, na kusihi, kwa machozi machoni mwake, mpaka Mungu amemsamehe dhambi zake, akaisafisha nafsi yake kutokana na maisha ya dhambi, na akamjaza na Roho Mtakatifu; akiwa na upendo mwingi sana, na utauwa, hata anavirudisha vile vyombo vya tairi hizo za zamani, alizoiba kutoka kwa majirani, kisha anaondoka anaenda kusahihisha mambo haya, na kuishi maisha ya kitauwa mbele za watu. Hatutakuwa na ufufuo kamwe katika nchi hii mpaka tutakapokuwa na mambo hayo. [Ndugu Branham amegonga mimbara mara nne—Mh.]

¹⁷⁹ Hukumu huanza katika nyumba ya Mungu, kwa Neno la Mungu. Amina. Si kitabu cha mafundisho, bali Biblia. Si kile makanisa fulani yanachofundisha katika theolojia zao, bali kile asemacho Mungu. Ndipo mtakuwa na ufufuo ambapo nguvu kuu, na maaajabu, na ishara, na miujiza, na cho chote kile, vitatukia.

¹⁸⁰ Sisi tuna uvuguvugu. Kwa maana tuna uvuguvugu katika wakati huu, Mungu alisema, “Nitawatapika mtoke katika kinywa Changu.” Wakati huu wa kanisa utakataliwa. Kutakuweco na mabaki yatokayo humo, ambao wataokolewa. Kwa hiyo ni afadhali ujichunguze mwenyewe, vizuri sana, kuona kama uko katika hayo mabaki sasa. Tutafikia jambo hilo mnamo dakika moja, Mungu akipenda. Angalia tu sasa.

Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu;

¹⁸¹ Ama, “vinara vya taa,” kinasema Kiyunani. Sasa, hiyo ni tafsiri ya kwanza, maana hawakuwa na mishumaa na ile... Walikuwa na vinara vidogo vya taa. Sasa, Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu, ndivyo tunavyoviita.

¹⁸² Naam, katika mahali patakatifu, ambapo ule mkate wa wonyesho; na wengi wenu enyi makasisi mnafahamu, na jambo hilo. Nanyi watu hapa maskanini, mkifundishwa na mwalimu mzuri hapa, mna—mnajua mambo haya.

¹⁸³ Vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu, vilikuwa... vilikuwa na taa ndogo juu yao, zilizotumia mafuta. Katika Zekaria, ambapo aliona lile ono, ninaamini lilikuwa ono, naye akaona mzeituni mwitu na mzeituni wa shambani; Wayahudi na Mataifa, kule nyuma kabisa kabla ya majira ya Mataifa. Wao walikuwa na vyetezo vya dhahabu, na vyetezo hivi viwili vya dhahabu viliingia kwenye moja ya hivi vinara vya taa hapa vilivyosambaza mafuta kwenye hizo taa zote. Naye asingefahamu jinsi mambo haya yalivyokuwa; mzeituni mwitu na mzeituni wa shambani. Nao huo mzeituni wa shambani, bila shaka, ulivunjwa, nao mzeituni mwitu ukapandikizwa ndani yake.

¹⁸⁴ Na mafuta hayo kwenye ile taa, *mafuta* yanawakilisha “Roho Mtakatifu,” daima. Tutafikia jambo hilo, juu ya alama ya watu, Ijumaa usiku. Angalia, lakini mafuta haya yanawakilisha Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu tunawatia mafuta wagonjwa, ni kwa sababu yanawakilisha Roho Mtakatifu.

¹⁸⁵ Biblia ilisema, katika Ufunuo sura ya 6, wakati mapigo yalipopita, alisema, “Kipimo cha ngano kwa dinari, na vipimo viwili vya shayiri kwa dinari; bali usiidhuru divai Yangu na mafuta Yangu.” Laiti tungalikuwa tunachukua Ufunuo wote, kwa majuma machache, na kuingilia jambo hilo, kwamba hiyo divai na mafuta ni nani. “Wala usiidhuru divai Yangu na mafuta Yangu! Usikaribie.” Amina.

¹⁸⁶ Sasa angalia vinara hivi vya taa vya dhahabu. Mafuta haya yalimwagwa kwenye vinara hivi vya taa. Sasa, mafuta ndiyo yaliyowekwa kwenye ile taa, ipate kuwaka. Sasa Haruni alikuwa... Ilikuwa ni wajibu wake kuwasha taa hizi. Nazo taa hizi zilipaswa kuwashwa. Shikilia jambo hilo sasa. Angalia. Iweni wenye kicho, mkasikilize. Taa hizi zilipaswa kuwashwa na moto ambao Mungu alikuwa amewasha. Wana wa Haruni waliingia na moto wa kigeni, naye Mungu akawaua mlangoni; hiyo ni kweli, moto wa kigeni. Moto alioanzisha Mungu!

¹⁸⁷ Basi angalia, sasa, vile vinara vya taa viliingia katika tao. *Hapa* kulikuweko na kinara kimoja cha taa, viwili, vitatu, vinne (juu kabisa), vitano, sita, saba, namna *hii*. Sasa, vinara hivyo vya taa vya dhahabu hapa...kama anavyosema katika dakika chache.

¹⁸⁸ Hebu tusome mbele kidogo, labda tutalipata. Nanyi msikilize aliyosema sasa. Vema. “Na kichwa Chake...” Naamini nimeenda mbele ya aya ya 12 pale, “Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu.”Aya ya 13:

Na katicakati ya vile vinara vya taa saba vya dhahabu nikaona mtu mfano... Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.

Kichwa chake kilikuwa kama—kama..nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu... nyeupe kama theluji; na macho yake... miali ya moto;

¹⁸⁹ Sasa hebu tusimame hapo kwa dakika moja tu, maana hatuwezi kuacha picha hiyo hapo namna hiyo tu. Angalia vinara hivi vya taa vikisimama hapa sasa. Sasa, vinara hivyo vya taa, kama tutakavyoona baadaye kidogo, vinawakilisha zile Nyakati Saba za Kanisa. Zinawakilisha Efeso, Pergamo, na kuendelea hata Philadelfia, kote kote mpaka Laodikia; Nyakati Saba za Kanisa.

¹⁹⁰ Na kila kimoja cha hivi vinara vya taa kilikuwa na chupa dogo ya mafuta imewekwa pale, na mafuta haya yaliwaka kwenye taa hii. Basi wakati taa moja ilipowashwa na moto wa Mungu, walichukua taa hiyo na kuiwasha hiyo nyingine, kisha wakaiweka chini; wakaiwasha hiyo nyingine; na moja ikawasha hiyo nyigine, kutoka kwa hiyo nyingine, kutoka kwa hiyo nyingine, hata ile taa ya mwisho. Angalia, mafuta yale yale!

¹⁹¹ Sasa Nyakati hizi Saba za Kanisa, zilianza na Efeso, na ‘Tira, Pergamo, na kuendelea. Naye Roho Mtakatifu, ambaye ni mafuta ya Mungu, alishuka juu ya kanisa hapo mwanzo, katika Efeso, Kanisa la Efeso, ambalo lilikuwa ni kanisa la neema. Ninyi Wabatisti mnapaswa kupiga makelele “amina” pale. Halafu juu ya kanisa la neema, ambalo katika Efeso, na barua ya Efeso inatutambulisha, kwamba tulikuwa nani kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Alishuka kule, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

¹⁹² Lakini ngoja kidogo, ndugu yangu Mbatisti, wao walimpokea namna gani? Walimpataje? [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara moja—Mh.] Kwa kujiunga na kanisa? La hashu. Walimpokea kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnasema, “Naam, Ndugu Branham, hiyo ni kweli.” Kulitukia nini kwako wakati alipokushukia?

¹⁹³ Angalia, Moto ule ule uliowasha mafuta pale, katika Efeso, uliyawasha katika ‘Tira; moto ule ule uliowaka kule, uliwaka katika Pergamo; ukawasha kote kote, mpaka Wakati wa Kanisa la Laodikia. Roho Mtakatifu yule yule, aliyewashwa na Mungu yule yule, kwa Moto ule ule. Nao Moto uliushuka katika Pentekoste umeiwasha taa, Kanisa, kwenye kila wakati, kote kote mpaka sasa.

¹⁹⁴ Lakini shida ya jambo hilo ni kwamba, sisi Wabatisti, sisi Wamethodisti, tuko *huku* nyuma kabisa, tukijaribu kuchukua jambo fulani la kihistoria, na hili hapa Kanisa likienda chini *hapa*. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo tumeachwa nyuma. Kila kanisa, wakati lilipoanza, hapakuwepo. . .

¹⁹⁵ Mwangalie Luther, katika yale matengenezo ya kwanza. Ni ufufuo wa jinsi gani, Luther! Angalia, nina kitabu chake cha mafundisho nyumbani. Jinsi ambavyo mtu huyo alitetemeka

chini ya Nguvu za Mungu! Jinsi alivyoamini katika kuponya Kiungu, akakukubali yeye mwenyewe; aliamini katika Nguvu za Mungu, hata kiasi kwamba, mpaka akanena kwa lugha, Martin Luther. Hiyo ni kweli kabisa. Martin Luther alinena kwa lugha wakati mwingine.

¹⁹⁶ Kisha wakati uliofuata ukaja, John Wesley. John Wesley alifanya jambo lile lile. Alipokuwa anahubibiri, alisema, “Ni maneno gani haya ninayonong’ona, nisiyoyajua mimi?” Hiyo ni kweli, akinena kwa lugha; aliamini katika kuponya Kiungu. Na hapo alipokuja Marekani, makanisa hapa yalimtenda kama yanavyowatenda watakatifu wanaojifingirisha, leo, walimtupa nje, makanisani. Nao walihubiri Injili huko nje, na kuanguka chini ya Nguvu za Mungu, mpaka wakalala sakafuni, usiku kucha wakati mwingine.

¹⁹⁷ Basi kitabu cha mafundisho cha John Wesley mwenyewe, nilicho nacho nyumbani sasa, ambapo alikuwa amepanda farasi siku moja, kumwomba mwanamke aliyekuwa mgonjwa, ndipo yule farasi akaanguka na mguu wake ukavunjika. Ndipo akashuka kwenye huyo farasi, akachukua chupa ya mafuta akamtia farasi mafuta, kisha akampanda akaenda zake. Moto ule ule ukiwaka kule!

¹⁹⁸ Bali nyinyi mmeushusha hata kwenye utaratibu fulani wa kanuni za dini, naye Roho Mtakatifu anasonga mbele. Sawa. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁹ Na katika kanisa la Kimethodisti, “Wana kasoro fulani,” vile... kitabu chao kilisema, “walipata mshtuko.” Nao wangeanza kutembea, nao wangeshikwa na mshtuko na kuruka, na kufanya namna hiyo, katika mikutano yao ya hema na kadhalika, hao Wamethodisti. Mbona, ndugu, kama John Wesley angaliweza kutokea jukwaani, angetahayari sana kwa ajili yenu, angewakana; isipokuwa awapige mijeledi mikali ya Injili aliyohubiri.

²⁰⁰ Nilisimama si muda mrefu uliopita, karibu na kaburi, mahali walipowafungulia hao mbwa wakubwa wakali, siku ile alipokuwa anahubiri juu ya Kuzaliwa upya, na kadhalika, na hayo. Ndipo lile kanisa kubwa la Uingereza likamfungulia hao mbwa. Ndipo akasema, “Jua halitashuka juu ya kichwa chako mara tatu, mpaka atakaponiita nikamwombee.” Naye akafanya hivyo; kisha akafa. Hiyo ni kweli. Hakika.

²⁰¹ Hilo ndilo tunalohitaji leo. Tunahitaji Methodisti ya namna hiyo. Tunahitaji Mbatisti mwingine kama John Smith, aliyekaa chumbani na kumsihi Mungu, na akaomba usiku kucha, hivi kwamba, hata macho yake yakavimba sana, asubuhi, mkewe angemwongoza mezani, apate kula.

²⁰² Loo, tunafanya nini leo? Kusimama pembeni, huku sigara iko mdomoni mwetu; na ni shemasi kanisani, kisha anashuka anaenda kucheza michezo ya kuigiza; kwenye sinema, na

kuangalia televisheni usiku kucha; na kutohudhuria kanisa; kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, kucheza bahati nasibu za mbio za farasi, na kujiita wenyewe Batisti. Upuuzi mtupu!

203 Tunachohitaji leo ni ufufuo mwingine wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, uliotumwa na Mungu. Amina. Simaanishi . . . Sijaribu kuwafanya mchochewe. Najua hamjachochea, lakini, ndugu, hiyo ni kweli. Kujaribu kuwaonyesha jambo. Ni kweli. Ndicho tunachohitaji. Vema.

204 Sasa, hiyo ni Biblia. Hivyo ndivyo Roho alivyosema, unaona. “Vinara vya taa.” Vema. Sasa ya ya 13.

Na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano . . . wa Mwana wa Adamu, . . .

205 Ati nini? Mmoja kama Yeye. Huyu alikuwa nani? Bibi-arusi Wake. Mmoja kama Yeye. Angalia jinsi ilivyokuwa.

. . . ameava vazi lililofika miguuni, . . .

206 Utakatifu wa Yesu Kristo ukimfunika Bibi-arusi. “Ametusafisha na dhambi zetu, kwa Damu Yake Mwenyewe.” Vema.

. . . kufungwa mshipi (si mwanamume; mwanamke) wa dhahabu matitini. (Injili ambayo ilishikilia Nguvu na utukufu wa Mungu juu ya Mwili wa Kristo!)

207 Loo, ni picha ya namna gani tunayofikiria hapa! Angalieni hapa.

. . . lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.

Kichwa chake na nywele zake ilikuwa nyeupe kama sufu . . . kama theluji (haki, utakatifu; ndivyo weupe unavyomaanisha); *na macho yake kama miali ya moto.* (Yanaangalia yote!)

208 Usijaribu kujificha toka Kwake. Yeye anajua u nani, mahali ulipo, na yale uliyofanya. Naam, bwana. Yeye anaona kila kitu. Ee, Mungu . . .

209 Tuna dakika chache tu zilizosalia, kufikia wakati huu mwingine wa kanisa, kama tukiweza. Angalia.

Na miguu yake ilikuwa kama shaba iliyosuguliwa sana, . . .

210 *Shaba* daima ni “hukumu,” mwajua; madhabahu ya shaba, na ile nyoka ya shaba, na kadhalika. Shaba inaonyesha hukumu. Miguu yake, basi, Kanisa la Yesu Kristo limekaa juu ya hukumu ya Kiungu. Kristo akifa badala yetu, yule Mwenye Haki akigharimia hukumu yetu kule juu, kwenye . . . mbele za Mungu, kisha akafa pale kama mwenye dhambi msalabani, nayo nafsi Yake ikashuka ikaenda kuzimuni. Ndipo Mungu, akikataa kuruhusu Mtakatifu Wake kuona uharibifu, alimfufua katika

siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu; Ambaye anaketi kwenye mkono Wake wa kuume sasa, Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; ambaye atarudi vivyo hivyo kama alivyopaa kwenda Mbinguni, kupokea Kanisa tukufu lililokwisha jitayarisha, lililosafishwa kwa Damu na kuzaliwa mara ya pili. Ni—ni ono la jinsi gani! Amina. Vema. “Kama shaba iliyosuguliwa sana,” ama, sasa angalia, “na ninii Yake . . . na . . .”

Na miguu yake ilikuwa kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba ilikuwa imesafishwa katika tanuru (yaani, taka zote zimeondolewa); na sauti yake . . . sauti ya maji mengi.

211 Angalia, hili ni kanisa linalozungumza Naye sasa, “maji.” Ufunuo 17:15, ilisema, “Maji yanamaanisha makutano na wingi wa watu.” Sasa, “Sauti Yake,” ama huyu Mwenye Hai aliyekuwa amesimama pale akiangalia namna hii, Kristo katika Kanisa Lake, kama Bibi-arusi na Kristo wakiwa mmoja, kama vile mume na mke ni mmoja; Kanisa na Kristo wakiwa wamefinyangwa pamoja kama Mtu mmoja, Roho Mtakatifu yule yule.

212 Na mambo yale aliyoyafanya Kristo, Kanisa pia linayafanya. Mnaliona? Hilo Kanisa linalopendeza pale katika utakatifu, katika Nguvu, katika ukuu, na kuona maono, ishara, maajabu. Kila kitu kama vile tu Yeye alivyofanya, hiki hapa duniani; likitoa sifa zote kwa Mungu, likisema, “Siwezi kufanya neno ila Baba anionyeshe Mimi; bali alinionyesha Mimi, na ndilo hili hapa.” Nao wanakuja kuyaona mambo haya yakitendeka.

213 Sasa, Kristo, akifinyangwa kuwa mmoja, “Na sauti ya maji mengi, watu wengi.” Si huyo mmoja tu; ilikuwa ni Kanisa zima, yale Makanisa Saba yakifinyangwa pamoja kuwa kitu kimoja katika Mwili mmoja mkuu uliokombolewa wa Bwana. Wamethodist, Wabatisti, Wapresbiteri, wote waliozaliwa mara ya pili walio na Roho Mtakatifu, wakinena kwa Nguvu za Mungu, huo ndio Mwili. Huo ni Mwili.

Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; . . .

214 “Kuume.” Kila kitu katika Biblia kina maana yake, mnaona.

. . . katika mkono wake wa kuume (sasa Yeye—Yeye ni Mfalme); na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking’aa kwa nguvu zake.

215 Naam, “Upanga mkali wenye makali kuwili unatoka katika kinywa Chake,” kutoka katika kinywa cha Huyu anayesimama pale, Kristo na Kanisa kama mmoja.

216 “Katika mkono Wake alishika nyota saba.” Nanyi mtaona mnamo dakika chake; ninataka kufikia jambo hilo, niache

Biblia iseme tu ilikuwa ni kitu gani. Ilikuwa ni wale wahudumu saba, mhudumu mmoja kwa kila wakati wa hizi Nyakati Saba za Kanisa, anakuja sasa, anawashika katika mkono Wake wa kuume. Amina. Huyu hapo. Kulikuwako na malaika saba, wajumbe saba, mmoja kwa kila kanisa. Mnaelewa?

²¹⁷ Hapo, Yeye anasimama pale, “Na Upanga mkali wenye makali kuwili unatoka katika kinywa Chake.” Upanga wenye makali kuwili ni nini? Waebrania sura ya 4, ilisema, “Neno la Mungu lina ukali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, hata kuingia kwenye mafuta ya viungo, na huyatambua mawazo ya moyo.” Vema.

Nami nilipomwona, nalianguka kwenye... nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho,

Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele, Amina. Nami ninazo funguo za mauti, na kuzimu. (Huyo ni Yesu. Sasa angalieni.)

Basi, uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na haya yatakayokuwa baada ya hayo. (Vema.)

Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, ni...mkono,...na ya vile vinara saba vya dhahabu. Zile nyota saba ni malaika saba wa yale makanisa saba;...

²¹⁸ Loo! Shikilieni jambo hilo. “Malaika saba ni wale wahudumu saba wa yale makanisa saba.” Kulikuwa na kanisa la kiongozi wa Efeso. Basi kama Mungu angeruhusu, nasi tungeendelea na jambo hili, na tusiingilie *Alama Ya Mnyama*, naweza kuwaonyesha kila mmoja wao, moja kwa moja hadi kwenye wakati huu wa mwisho, wa—walikuwa ni akina nani; niwaonyeshe Kanisa la Filadelfia, ambalo lilikuwa ni Wamethodisti, John Wesley; niwaonyeshe Ka—Kanisa la Thiatira, mara baada ya Pergamo; ambaye alikuwa ni Martin Luther, na kuendelea kushuka moja kwa moja kwenye kila wakati, na kuwaonyesha kila mmoja wao aliyekuja na kuleta ujumbe, kuanzisha ujumbe duniani.

²¹⁹ Na moja kwa moja hata kwenye Ujumbe wa mwisho, leo, hiyo ni kweli, ambapo Mungu alimtuma malaika kutoka Mbinguni, akamthibitisha mtumishi Wake, na kutuma Ujumbe kwa kila mmoja. Hili halitakuwa kanisa. Halitakuwa madhehebu kwenye siku hizi za mwisho. Maana, Mungu ameweka madhehebu kwenye rafu, nanyi nyote mna habari na jambo hilo. Basi ngojea mpaka kesho usiku tutakapomaliza, juu ya *Alama Ya Mnyama*, tuone mahali kanisa lenu lilipo, mnaona, na madhehebu yako.

Sasa angalieni yale makanisa.

...Zile nyota saba ulizoonna ni yale makanisa saba;
(Hayo ni makanisa.)

220 Na “zile nyota,” ambazo, Yeye anashikilia kila nyota. Sasa angalieni. Tungeweza kukoma kwa dakika moja tu? Najua nimebakiza kama dakika kumi na mbili hapa nami nataka kufika kwenye sura hii papa hapa, na kusoma yote, hata kama sifanyi lo lote lingine. Nataka kuwaeleza jambo hili. Nyota ilikuwa ni mhudumu, na mhudumu aliyetiwa mafuta na Roho itokayo Juu.

221 Unatambua ya kwamba wewe unawakilisha nyota Mbinguni, na kila nyota Mbinguni inakuwakilisha wewe? Ulijuua Mungu alimwambia Ibrahimu ya kwamba mzao wake ungekuwa kama nyota za Mbinguni? Kwanza walikuwa ni mavumbi ya nchi, halafu katika ufufuo walikuwa nyota za Mbinguni, hawahesabiki. Ulitambua jambo hilo?

222 Je, ulijua Yesu alikuwa Nyota Yenye Kung’aa ya Asubuhi Inayong’aa, Nyota iliyo kubwa sana kuliko nyota zote za Mbinguni? Loo, haleluya! Ninapowazia jambo hilo, nafsi yangu inaruka kwa furaha. Huyu hapo! Huyu hapo katika sura Yake, katika Uwepo Wake, tutaketi siku moja, haleluya, wakati mambo ya dunia hii yatakapokuwa yamepita.

223 Lakini, sikilizeni, Andiko lingine linanijia. Danieli alisema... Wakati aliposema, “Yafunge...”

224 “Hapo alipomwona Malaika huyu akishuka, na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake; akaweka mguu mmoja juu ya nchi, na mwingine juu ya bahari; kisha akainua mikono Yake, akaapa kwa Yeye aliye hai milele na milele. Wakati sauti hizo saba zilipotoa ninii zao... Zile Ngurumo Saba zilipotoa sauti zao.” Yeye alisema, “Zitie muhuri; hazitajulikana mapaka siku ya mwisho.” Alisema, “Lakini wakati siri hii ya Mungu itakapotimizwa, wakati hizi zitakapofunuliwa kwa Kanisa; kisha akaapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba hapatakuwapo na wakati baada ya haya.”

225 Sikilizeni aliyosema pale basi. Alisema, “Nenda zako, Danieli, kifunge Kitabu.” Mnaona? “Kwa maana wewe utastarehe, nawe utasimama katika siku za mwisho, katika kundi lako. Lakini hao wawaongozao wengi kutenda haki watang’aa kuliko nyota, milele na milele.”

226 Hizo hapo, “nyota,” hao wahudumu saba. Wahudumu saba, katika Nyakati Saba za Kanisa, ambazo zinachukua miaka elfu mbili.

227 Toka miaka elfu mbili ya kwanza, yale maangamizi yaliyotangulia siku za gharika; miaka elfu mbili ya pili, kuja kwa kwanza kwa Kristo; miaka elfu mbili ya tatu, ya sita, ni kule Kuja kwa pili kwa Kristo; na ule Utawala wa Miaka Elfu, na ule mwisho, ile raha ya siku ya saba.

228 “Kwa kanisa...” Loo, mtanivumilia kwa dakika chache zaidi? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Nami sitaki kuwachosha, bali nitasoma haraka sana sasa. “Kwa malaika...” Sasa angalieni, Yeye ananena haya moja kwa moja sasa. Nasi tutaenda Pergamo na kupata lile lao la mwisho basi... Ninamaanisha, kwa la Laodikia, kisha tutafunga. Kesho usiku tutaendelea kutoka hapo, juu ya *Alama ya Mnyama*.

Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso... (lile la kwanza)

229 Sasa angalia, wakati Yesu alipokuwa amesimama ameinua mikono Yake. Hapa kuna kitu kidogo nisichotaka kuacha, kwenu. Kisikilizeni. Kiangalieni. Yeye anasimama katikati, yaani katikati, ya vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu.

230 Sasa, kama nilikuwa nimesimama *hapa*, na vinara vya taa vimefanya tao kunizunguka, *hapa* kwenye mkono wangu mmoja ndiko nimekishika, na *hapa* kuna kingine, katika mfano wa msalaba, maana Kanisa lililetwa kwa njia ya msalaba.

231 Huyu hapa amesimama; na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, kama agano. “Nimefanya agano Langu na Kanisa, kwa njia ya Ibrahimu, kwa njia ya Mzao wake, wote walioitwa.”

232 Ndugu yangu, usiku wa juzijuzi, akimpokea Kristo, alisema, “Usinisukume kamwe, Bill.” Kasema, “Wakati Mungu anapozungumza nami...”

Nikasema, “Huwezi kuja mpaka akuite.”

233 “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu.” Mtu mwingine anafanya kitu kingine, anakuvuta, huyo ni mtu mwingine. Lakini wakati Mungu anaponena, utakuja, unaona. Hiyo ni kweli. Nikisimama pale...” Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu.”

234 Huyu hapo amesimama pale, “alionekana mithili ya jiwe la akiki na yaspi, wa kwanza na wa mwisho,” Benyamini na Reubeni, wale wazee wetu wote kumi na wawili. Na jinsi, Biblia, kila sehemu inaumana moja kwa moja pamoja namna hiyo, kila kitu kikamilifu! Angalia wakati Yeye anasimama pale, mithili yake sasa, angalia kinachotukia. Yeye alisema alikuwa “Alfa na Omega,” alikuwa “wa Kwanza na wa Mwisho. Yeye Aliyekuwako, na Aliyeko, na Atakayekuja.” Alishika katika mkono Wake wa kuume, sasa, zile nyota saba.

235 Sasa hapa alianza katika Efeso, Naye anaanza kukiwasha kinara cha taa. Alikiwasha pale. Halafu wakati uliofuata, tunaona, wakati wa kanisa uliofuata, ikaanza kufifia; wakati wa kanisa uliofuata inafifia zaidi kidogo; mpaka wakati wa nne wa kanisa, ile miaka elfu moja mia tano ya nyakati za giza. Na yapata mwaka wa 500, 1500, katika wakati huo hapo, ikaanza kuwa giza hata ikawa iko juu kabisa, karibu izimike.

²³⁶ Pia, angalieni, kila moja ya nyakati hizo za kanisa, Yeye alisema, “Hamjalikana Jina Langu. Hamjalikana Jina Langu. Hamjalikana Jina Langu.” Lakini wakati anapotokea upande ule mwingine wa nyakati za giza, alisema, “Una jina, ulisema una-‘ishi,’ nawe umekufa.” Lilikuwa limeunda madhehebu. Likachukua jina lingine, jina la uongo.

²³⁷ Angalia, kesho usiku, vile mpinga Kristo alivyo. Yeye ana ubatizo wa uongo, akikufanya uamini ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yeye ana ubatizo wa uongo wa maji, naam, bwana, ambao hata si wa Kimaandiko. Yeye ana mambo hayo yote, ya kutosha tu kuiga, kuwa mjanja na mwerevu.

²³⁸ Angalia mahali jambo hilo linapotokea. Papo hapo ndipo lilipoanzia, papo hapo; linatokea upande huu mwingine *huku*.

Kisha Yeye akasema, “Una nuru ndogo tu,” Luther.

²³⁹ Kisha moja kwa moja akaja Wesley, na jinsi ilivyokuwa katika wakati wake. Ikaanza kuangaza.

²⁴⁰ Halafu, tokea katikati ya wakati huo na wakati wa mwisho, Yeye aliweka mlango uliofunguliwa. Ameweka mlango uliofunguliwa kwa ajili ya wale ambao wangeingia. Kisha akasema, “Lilianguka katika hali ya uvuguvugu.” Ndipo akalitapika kutoka katika kinywa Chake. Akachukua ya mabaki, halafu ufufuo ukaja, Naye akaondoka pamoja nao. Hiyo ni kweli.

²⁴¹ Huyu hapo, amesimama katikati ya vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu. Sasa:

Kwa . . . kanisa lililoko Efeso andika;

Mambo haya andika, haya ni yale anenayo yeye azishikaya hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu.

²⁴² “Nayajua matendo yako.” Kumbuka, hayo hayakusahauliwa.

Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na . . . huwezi kuchukuliana na watu wabaya, . . .

²⁴³ Nasi tunachukuliana tu na kila kitu ambacho ni kibaya, na kukiita dini. “Loo, vema, wao wanaenda . . . Tunahudhuria kanisa. Sisi ni wema kama tu hao jamaa wengine.” Wanaenda moja kwa moja nyumbani, wanakaa nyumbani Jumatano usiku na kuangalia televisheni, ambayo ndiyo shimo halisi la kuzimu. Hiyo ni kweli. Nao wanatoka moja kwa moja wanaenda kusikiliza kwenye sinema, kwenye sinema za kutazama ukiwa kwenye gari. Ni joto sana kwenda kwenye sinema, hata . . . kwenda kanisani; na hata mhubiri anafunga, katikati ya msimu wa kiangazi. Mnasema, “Ni joto sana kwenda kanisani.” Si kubaya sana, kwenda kuzimu, ndugu. Utaenda, moja ya siku hizi, ambako ni joto zaidi ya huko. Afadhali usikilize.

244 Unawezeje? Ndugu, usingeweza kumfanya hua kula mzoga wa farasi, hata ukifanya nini. Asingeweza kufanya jambo hilo. Tabia yake ni tofauti. Hua hana nyongo. Hawezi kuuyeyusha tumboni.

245 Naye mtu aliyezaliwa mara ya pili, kwa Roho wa Mungu, hawezi kula vitu hivyo. Hawezi kuvivumilia. Haviko kwenye mawazo yake. Hawezi kufanya jambo hilo. Hawezi.

246 Unajua jambo hilo. Kila ndege na wimbile. Basi, leo, ulimwengu na kanisa vimefanana sana, ninyi... Wao wanazungumza vile vile, wanakunywa pombe vile vile, wanavuta sigara vile vile, wanalaani vile vile, wanavalia vile vile, wanatenda vile vile. Nao, huwezi kuwatofautisha, nanyi inadhaniwa kwamba mmejazwa na Roho Mtakatifu.

247 Hilo ni zito sana, ndugu, lakini, nawaambia, litawapa Uzima.

248 Kulikuwako na jamaa fulani, wakati mmoja, alienda kwenye kundi la wahubiri, mahali walipokuwa na seminari, iliyoitwa shule ya manabii. Ndipo mmoja wao akasema, “Weka ile sufuria kubwa sasa. Tutakula chakula cha jioni.” Kasema, Eliya yuaja, mtu ambaye kweli ana sehemu maradufu.”

249 Kwa hiyo mmoja wa jamaa hao akatoka akaenda kuchuma baadhi—baadhi ya njengere, naye akajaza nguo yake matango mabichi kisha akayatia katika sufuria, akaanza kuzichemsha. Mbona, wao wakaanza kula. Wakasema, “Mauti imo kwenye sufuria.” Jambo hilo ni kama tu baadhi ya seminari hizi wanazobuni, pia. Hiyo ni kweli. Kasema, “Kuna mauti kwenye sufuria.”

250 Eliya akasema, “Ngojeni kidogo, tunaweza kushughulikia jambo hilo.” Anaondoka anaenda anachukua konzi moja ya unga, anaitupa mle ndani, kwa hiyo hilo likabadilisha mambo. Unga, sadaka ya unga, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” mbegu zenye miiba zilizosagwa namna ile ile, kwa ajili ya sadaka ya unga, na jambo hilo lilileta tofauti.

...huwezi kuwavumilia watu wabaya, tena
umewajaribu wale wajiitao wahubiri, ama mitume,
nao sio, ukawaona kuwa waongo;

251 Hivyo ndivyo alivyosema; mimi sikusema jambo hilo. Mimi ninamnukuu Yeye tu. Bali mnajua anachohitaji Mungu? Mungu anahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, la sivyo umepotea.

252 Basi mtu hapa aliye na baadhi ya hizo D.D.D., na ma-L.D., na za Ph.D, na Digrii ya Sanaa, na cho chote kile nyuma ya hiyo, na wakati mwingine hajui lo lote juu ya Mungu. Hiyo ni kweli. Ndugu, hiyo haimaanishi kitu cho chote. Lakini ulimwengu mzima unasema, “Lakini, mhudumu wetu ni Daktari wa Theolojia.” Loo, rehema! Hilo halina uhusiano wo wote na Mungu kuliko—kuliko kunywa maji; si zaidi ya hivyo. Hilo ni

kweli. Mungu hajali ni Ph.D. ngapi, ama D.D. ngapi. Nawe—nawe wajua kile Biblia inachoita. . . Sasa, huu si utani, maana siamini katika kutaniana. Lakini Biblia inaita D.D., “mbwa mfu.” Hivyo ndivyo Biblia ilisema ilikuwa hasa, “mbwa mfu.” Vema, kasema, “Wao hawawezi kubweka.” Kwa hiyo, basi, vema.

Tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu. . .

253 Loo, nataka kusesitiza jambo hilo, ili kwamba mpate jambo hilo katika siku chache usiku, Mungu akipenda.

. . . na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka.

254 “Ulidumu Nalo tu.” Vema. Angalia.

Lakini nina mambo machache juu yako, . . .

255 Sasa hapa ndipo nitakapoachia sasa, kwa muda kidogo, mpaka nitakapopata jambo hili papa hapa ili tupate kulishika kesho usiku.

Lakini nina mambo machache juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.

256 Kuna nini maskanini? Mtu anapaswa kuweza kusema, unapokutana na mtu, ni. . . Maisha yako ya Ukristo, ni lini yalikuwa mazuri zaidi ya yote kwako? Unapaswa kuweza kusema, “Sasa hivi!”

257 “Vema, tukio langu lililo zuri kuliko yote lilikuwa kule nyuma nilipopata ubatizo wa Roho Mtakatifu mara ya kwanza, nilipokuja.”

258 Sema tu, “Loo, ndugu, umeanguka kutoka kwenye neema.” Hiyo ni kweli. Angalia, “Umeacha upendo wako wa kwanza,” ikionyesha ya kwamba walikuwa na kitu fulani hapo mwanzo, nao wamekiacha.

259 “Si yeye aanzaye; bali yeye avumiliaye hata mwisho, huyo ataokolewa.” “Si wote wasemao, ‘Bwana, Bwana,’ bali wale watendao mapenzi ya Baba Yangu.” Loo, hebu tuache hilo lizame kwa dakika chache. Nilikuwa ninazungumza haraka usiku wa leo, hata hivyo, kwa hiyo hebu tuache jambo hilo lizame kwa dakika chache tu, mnaona. “Yeye atendaye mapenzi ya Baba Yangu.” “Yeye avumiliaye hata mwisho. Yeye avumiliaye!”

260 Kama mtu fulani akisema, “Ninaamini huyo, huyo jamaa, ni mnafiki wa kale.”

261 “Vema, kama unafikiria jambo hilo juu yangu, nitaacha kanisa. Sitakuwa na uhusiano wo wote nalo.” Vema, haya basi. Mnaona? Inaonyesha umefanyizwa kwa kitu gani. Lakini kama ingalikuwa ni ngano mwanzoni, itakuwa ni ngano mwishoni. Hukukaa tu muda mrefu wa kutosha huku chini. Hukusahihisha jambo hilo. Hiyo ni kweli.

Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; . . .

262 Rudi nyuma na ukumbuke wakati ulipokuwa na yale maisha ambapo usingemsengenya mtu ye yote. Wakati kitu cho chote kilichoenda kombo kanisani, hukuketi kwenye vipandio vya jirani yako kule na kulisengenya kanisa, na kumsengenya kila mtu, ukakimbia kwenda kujiunga na kanisa lingine. La, ulikaa pale pale, ukaomba kabisa kwa subira, ndipo Mungu akalitatua jambo hilo, unaona.

...kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu,...

263 Mnajua maana ya “kutubu,” sivyo?

ukayafanye matendo ya kwanza...

264 Rudi nawe ukapate lile tukio lako la kwanza. Fanya mambo yale uliyofanya hapo awali. “Nenda madhabahuni ukalisawazishe jambo hilo na Mungu,” kwa maneno mengine. Hiyo ni kweli.

...ukafanye matendo yako ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako upesi, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.

265 A-ha, “Usipofanya jambo hilo, utakuwa na kanisa lililovunjika, na kuvurugika vipandevipande, ’sipokuwa wewe utubu.”

266 “Lakini jambo hili wewe...” Loo, sasa sisi hapa tunakuja. Sikilizeni sawasawa. Sikilizeni kwa makini. Vaeni fulana zenu za kidini sasa, kisha mshushe mwamvuli wenu. Sikilizeni. Kwa kuwa...

Lakini unalo neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Nikolai, ambayo na mimi nayachukia.

267 “Wayachukia matendo ya Mnikolai.” Sasa angalia. Yale yaliyokuwa ni “matendo” katika Efeso, katika wakati wa kanisa uliofuata yalikuwa “mafundisho.” Tutachukua jambo hilo, kesho usiku, “Nikolai.”

Basi yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye, Mimi nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.

268 Sasa, aya inayofuatia, aya ya pili inaanza na Kanisa la Smirna.

269 Sasa, “Nikolai,” hapo ndipo tutakapoanzia, kesho usiku, kutoka katika Ufunuo 13. Ukuhani wa Kinikolai, jinsi ulivyoanza moja kwa moja kule Efeso. Na hapo ndipo huo wakati wa kanisa uliposhindwa, katika miaka mia tatu ya kuweko kwake. Kabla haujaisha, Wanikolai walianza kuanzisha fundisho fulani, ukuhani wa ndugu.

270 Na basi, kwanza, ulitoka kwa Nikolasi, ambaye alikuwa mmoja wa—wa mitu—...mmoja wa wale...naye...Katika Matendo sura ya 6, naamini, na aya ya 5, ambapo aliondoka

akaenda akawachagua mashemasi. Nao wakamchukua huyu, ambaye alikuwa Nikolasi pale, na wakaanza kutoka mahali pale na kuuita Unikolai, nao wakaanza kufanya ukuhani. Basi kutoka hapo ukawa “matendo,” waliyokuwa wanafanya, wakisema mambo haya kwa maungamo, na kadhalika. Na kisha yakawa “fundisho” upande huu, ndipo likaingia Babeli. Nalo likaishia huku, kwenye wakati wa mwisho, huku Ukristo wote umefungiwa kwake; ni wachache tu wamebaki watakaookolewa kutoka kwake. Angalia uone ni kitu gani, kesho usiku, Mungu akipenda.

²⁷¹ Loo, ndugu yangu mpendwa, dada yangu mpendwa! Kwake Yeye anayeweza kukuzuia usianguke, Kwake Yeye anayeweza kuushikilia moyo wako katika neema, na azimwage baraka Zake juu yako. Naomba usisahau ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho za wakati wa mwisho wa kanisa, ambao umebashiriwa kuwa wakati wa kanisa wenye uvuguvugu, mlegevu tu kwa Jambo hilo. Basi acha kuwa mlegevu! Njoo kwa Kristo kabisa, kwa moyo wako wote.

²⁷² Sikwambii ujiunge na kanisa gani. Hilo halina... Mungu hatakuuliza jambo hilo kamwe kwenye ile Hukumu. La, bwana. Yeye hajali wewe ni wa kanisa gani.

²⁷³ Yeye anakutaka *wewe*; ni mtu binafsi. Nawe huna budi kuzaliwa mara ya pili na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, la siyo umepotea. Unaona? Wewe unajifanya mwaminio, unaiga tu, mpaka umepokea tukio la kuzaliwa mara ya pili.

²⁷⁴ Na, sasa, Yeye aliyesimama pale, na vile Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu, kupitia Nyakati Saba za Kanisa; na Roho Mtakatifu yeye yule aliyeliwasha Kanisa pale, analiwasia hapa.

²⁷⁵ Sasa, kumekuweko na waigaji katika kanisa hilo, na hawa Wanikolai pale, na kote kote katika kila wakati wa kanisa, waigaji, mpaka inafikia hapa mpaka inakuwa lundo moja kuu mno la madhehebu. Ndipo Mungu anakitupa nje kitu hicho chote kizima, kisha anayachukua mabaki ya watu Utukufuni.

²⁷⁶ Bwana na awabariki. Hili kwa namna fulani linaparuza, enyi marafiki, lakini ni zuri. Litawasaidia na kuwazuia kuanguka. Sasa, msiende kila mahali, mkisema, “Ndugu Branham alilitupilia kanisa langu mbali.” Hilo halikukusudiwa kwa kanisa lo lote. Lilikusudiwa kwa ajili yako tu, kama mtu binafsi. Mimi si...

²⁷⁷ Kama wewe ni mfuasi wa kanisa la Kibatisti, basi kuwa Mbatisti halisi aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Kama wewe ni wa kanisa la Kimethodisti, uwe Mmethodisti halisi aliyejazwa na Roho Mtakatifu, lo lote lile. Nawe hutawiwa; utakuwa na sifa njema kwa kanisa lo lote, ama ujirani wo wote, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Bwana na awabariki sasa, tunaposimama, mkitaka.

278 Bwana Mpendwa wa Uzima, baada ya kulisoma Neno Lako, tunasimama katika uchaji. Tukitambua ya kwamba siku moja kusoma huku usiku wa leo kuta... Tutakusikia katika kanda zilizorekodiwa, tuseme, kwenye Siku ya Hukumu. Tutafanyaje juu ya jambo hilo? Kuona ya kwamba tunaishi katika wakati huu wa mwisho, giza kila mahali, ni wakati wa namna gani! Kuona kule Kuja kwa Bwana, ishara zikitokea, “mawimbi makubwa ya maji yakivuma; watu wakivunjika mioyo; hofu, mshangao wa wakati; dhiki kati ya mataifa.”

279 Wengi wanasema, “Loo, nimesikia jambo hilo kwa miaka kadha.” Lakini hivi Maandiko hayakusema wangesema ya kwamba, “Hakuna tofauti na wakati baba zetu walipolala”? Bila kujua ya kwamba tuko mlangoni kabisa. Yeye anaweza kuja kabla ya asubuhi.

280 Basi, Baba, ni siku ya namna gani ama ni majira ya namna gani, tunayojua, ambapo nyuzi hizi ndogo za maisha tunazotembea juu yake zitakatika kutoka chini yetu. Maskini nafsi zetu zitaning’inia kule kwenye mizani, kwenye Neno la Mungu, na misimamo yetu ya yale tumesikia na kusoma.

281 Inatupasa, Bwana, kusimama sasa na kujichunguza wenyewe. Na wakati wanaume na wanawake, wavulana ama wasichana, tukisimama hapa katika kusanyiko hili dogo, usiku wa leo, wenye akili timamu na wenye busara, na wafikirie kwa makini sasa hivi. Na iwapo hawajazaliwa mara ya pili, na wakusudie moyoni mwao sasa hivi, “Mimi sitakula wala kunywa mpaka utakaponijaza na mana uliyowajaza nayo katika Siku ya Pentekoste. Mpaka ulimwengu unakuwa umekufa, na kila kitu kiwe cha pili ila Wewe, Bwana Wangu, na upendo wa kitu kingine cho chote utatoweka. Bali ondoa upendo wote wa ulimwengu kutoka kwangu, na nijalie tangu leo niwe Wako kabisa.” Lijalie, Bwana.

282 Uandamane na watu wanapoenda manyumbani mwao. Wakumbuke wenye haja, Ee Mungu, walio maskini nchini mwetu, walio maskini wa roho, hao walio na njaa.

283 Mungu, wainue wahudumu, kila mahali. Wajaze na Roho Mtakatifu, na uwatume, wakihubiri, Bwana, kama minge. Hatujui ni wakati gani... Tunapita njia hii mara moja tu. Sisi huwa binadamu mara moja tu, na Mungu ashukuriwe kwa jambo hilo. Lakini, maisha yafuatayo, hatutaihubiri Injili katika maisha yajayo; bali tutafurahi katika Injili, pamoja na hao wa nyakati hizo ambao wamelikubali Hilo; pamoja na Jemadari Mkuu, Bwana wetu Yesu Ambaye anastahili kabisa, na sifa zote ziwe Kwake milele na milele. Amina.

284 Mungu awabariki. Geukeni mkapeane mikono ninyi kwa ninyi, huku tukiimba *Kibarikiwe Kifungo Kitufungiacho*. Kama ninyi...

Kibarikiwe kifungo
Kitufungiacho mioyo,
Ushirika wetu wa fikira zetu
Ni kama wa Mbingu.

Mbele ya Enzi ya Baba,

²⁸⁵ Sasa peaneni mikono mmoja kwa mwingine. Ni dakika kumi tu, ule wakati, kwa maana nuru sasa zinapokezanwa. Nyote peaneni mikono, mwende nyumbani, mkifurahi, kisha mrudi kesho usiku. Kwenye saa moja na nusu, kamili, tutaanza ibada, Mungu akipenda. Inapendeza jinsi gani!



NYAKATI SABA ZA KANISA SWA54-0512
(The Seven Church Ages)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, Mei 12, 1954, Katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org